

**KUCHUNGUZA MATUMIZI YA TAFSIDA KATIKA LAHAJA YA**

**KIPEMBA: UCHUNGUZI WA MAZUNGUMZO**

**MAUA AME YUSSUF**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA MASHARTI**

**YAKUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI - ISIMU) YA**

**CHUO KIKUU HURIACHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kuwa amesoma tasnifu hii itwayo:  
**Kuchunguza Matumizi ya Tafsida Katika Lahaja ya Kipemba: Uchunguzi wa Mazungumzo**”, na ameridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili (M.A.Kiswahili - Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Dkt. Anna Kishe

(Msimamizi)

.....

Tarehe

**HAKIMILIKI**

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile ya Tasnifu hii kama kutoa sehemu ndogo ya tasnifu hii, kielektroniki au njia nyengine yoyote ile bila ya idhini ya Muandishi wa Tasnifu hii au kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## **TAMKO**

Mimi, **Maua Ame Yussuf**, natamka na nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine ile.

.....

Sahihi

.....

Tarehe

**TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa mtoto wangu Fatma Hamad Abdallaili iwe kwake ni chachu  
ya kujali elimu na kujifunza kwa bidii.

## SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba wa ulimwengu na vilivyomo na kunipa uwezo wakufanya utafiti huu, kuandika na kukamilisha. Pili napenda kuwashukuru wote waliochangia kwa namna moja ama nyengine kukamilika kwa kazi hii. Hata hivyo si rahisi kuwataja wote kwa majina, ila napenda kuwashukuru wote nitakaowataja na ambao hawakutajwa kwa mchango wao wa kuifanikisha kazi hii.

Shukurani za pekee ziende kwa msimamizi wangu Dkt Anna Kishe kwanza kwa kuwa karibu nami, lakini pia kukubali kuwa msimamizi wa kazi yangu na mwisho kuniongoza kwa kila palipostahili kuongozwa juu ya kazi yangu hii hadi kukamilika kwake. Mungu amzidishie upendo na nguvu za kusaidia wengine wote wanaotaka msaada kutoka kwake.

Shukurani nyingine ziende kwa Mlezi wa Chuo Kikuu Huria Tawi la Pemba, Mwalim Bakari Kombo kwa kuwalea wanafunzi na kuwasaidia kwa hali na mali ili kukamilisha lengo lao la kujipatia elimu. Mungu amlipe wema huo.

Pia naishukuru familia yangu kwa kuwa pamoja na mimi bega kwa bega tangu mwanzo wa kuanza masomo hadi kukamilika kwake na kunisaidia kwa hali na mali, familia hiyo akiwemo kwanza Mume wangu Hamad Abdalla Ali ambae ni muhimili mkuu wa kunisiadia kwa

Kustahamili katika kipindi chote kigumu lakini pia kunipa mawazo yanayofaa juu ya mchakato wa kujisomea. Wengine ni kaka zangu Juma Ame Yussuf, Moh'd

AmeYussuf na Omar AmeYussuf kwa kunipa moyo na ari ya kujiendeleza kimasomo, pia bila ya kumsahau Dada Khadija Kombo kwa kuweza kunipa mawazo na kunikwamua pale nilipokwama ili kuendelea mbele juu ya wote hao siwezi kumsahau Mama mzazi Siti Moh'd Shaame kwa kuwangoza wanawe wote juu ya kutodharau suala la elimu na pia kuwapa malezi bora ambayo yalitusaidia katika maisha yetu hadi leo nathubutu pia kusema Allah awalipe wema wao huo wote.

Aidha ninaushukuru uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na wanataaluma wenzangu wa kitivo cha Sanaa na Sayansi ya jamii kwa kunishawishi na kunihimiza kuikamlisha kazi yangu hii. Nasema kwa pamoja Ahsanteni sana.

Allah ndie muweza wa kila kitu.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulihusu *Kuchunguza Matumizi ya Tafsida Katika Lahaja ya Kipemba*. Mtafiti alichagua mada hii ili kuchunguza na kuchambua utajiri mkubwa wa tafsida za lahaja ya kipemba zinavyotumika kwa Wapemba wenyewe. Utafiti huu una lengo kuu moja na malengo mahsusi matatu. Aidha mtafiti alitumia nadharia moja tu nayo ni nadharia ya *Simiotiki*. Pamoja mtafiti alitumia njia nne za kukusanyia data nazo ni usaili, Uchunguzi makini, Hojaji na mbinu ya maktabani. Data za utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo, Uchambuzi wa dada ulifanyika kulingana na madhumuni mahususi yaliyotajwa ndani ya utafiti huu. Utafiti umegundua kuwa zipo tafsida za lahaja ya kipemba ambazo hutumiwakwa lengo la kuleta heshima katika mazungumzo ya wapemba, lakini pia kulinda na kuendeleza utamaduni wa Wapemba kwa kuzitumia vyema tafsida hizo. Mtafiti amegundua matumizi tofauti ya tafsida ambazo zinatumika na kuleta heshima katika mazungumzo, tafsida hizo ni kama vile *kubaua, kujisaidi, utupu/ushi, msalani, kujamiiana (Kuingiliana), mja mzito* na mengineyo. Mwisho matafiti amehitimisha kazi yake kwa kutoa mapendekezo kwa wasomi, walimu na wanajamii kwa ujumla kwa kuzilinda na kuziendeleza tafsida, pia kuandaa tafiti nyingine zinazohusu tafsida kupitia lahaja na lughanyingine za makabila.



## YALIYOMO

|   |             |
|---|-------------|
| <b>UTHIBITISHO .....</b>  | <b>ii</b>   |
| <b>HAKIMILIKI.....</b>  | <b>iii</b>  |
| <b>TAMKO .....</b>  | <b>iv</b>   |
| <b>TABARUKU.....</b>  | <b>v</b>    |
| <b>SHUKURANI .....</b>  | <b>vi</b>   |
| <b>IKISIRI .....</b>  | <b>viii</b> |
| <b>ORODHA YA VIAMBATANISHI .....</b>                            | <b>xiii</b> |
| <b>SURA YA KWANZA .....</b>                                     | <b>1</b>    |
| <b>UTANGULIZI WA JUMLA.....</b>                                 | <b>1</b>    |
| 1.1 Utangulizi .....  | 1           |
| 1.2 Usuli wa Mada .....   | 1           |
| 1.3 Tatizo la Utafiti .....                                     | 4           |
| 1.4 Malengo ya Utafiti .....                                    | 5           |
| 1.4.1 Lengo Kuu.....  | 5           |
| 1.4.2 Malengo Mahasusi .....                                    | 5           |
| 1.5 Maswali ya Utafiti.....                                     | 6           |
| 1.6 Umuhimu wa Utafiti Huu.....                                 | 6           |
| 1.7 Mipaka ya Utafiti .....                                     | 7           |
| 1.8 Hitimisho.....  | 7           |
| <b>SEHEMU YA PILI .....</b>                                     | <b>8</b>    |
| <b>MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA .....</b> | <b>8</b>    |
| 2.1 Utangulizi .....  | 8           |
| 2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi .....                             | 8           |

|                              |   |           |
|------------------------------|---|-----------|
| 2.2.1                        | Dhana ya Tamathali za Semi.....                 | 8         |
| 2.2.2                        | Dhana yaTafsida.....                            | 10        |
| 2.2.3                        | Dhana ya Lahaja.....                            | 12        |
| 2.4.4                        | Kazi Tangulizi Kuhusu Tafsida .....             | 12        |
| 2.2.5                        | Kazi Tangulizi Kuhusu Tamathali za Semi .....   | 14        |
| 2.2.6                        | Kazi Tangulizi Kuhusu Lahaja za Kiswahili ..... | 16        |
| 2.3                          | Pengo la Utafiti .....                          | 17        |
| 2.4                          | Mkabala wa Nadharia .....                       | 17        |
| 2.4.2                        | Nadharia ya Simiotiki .....                     | 17        |
| 2.5                          | Hitimisho.....                                  | 18        |
| <b>SURA YA TATU .....</b>    |   | <b>19</b> |
| <b>MBINU ZA UTAFITI.....</b> |   | <b>19</b> |
| 3.1                          | Utangulizi .....                                | 19        |
| 3.2                          | Eneo la Utafiti .....                           | 19        |
| 3.3                          | Mbinu za Kukusanyia Data .....                  | 19        |
| 3.3.1                        | Usaili .....                                    | 20        |
| 3.3.2                        | Uchunguzi Makini.....                           | 20        |
| 3.3.3                        | Mbinu ya Hojaji .....                           | 21        |
| 3.3.4                        | Mbinu ya Maktabani .....                        | 21        |
| 3.4                          | Mbinu ya Uchambuzi wa Data.....                 | 22        |
| 3.5                          | Usampulishaji.....                              | 22        |
| 3.6                          | Sampuli .....                                   | 22        |
| 3.7                          | Hitimisho.....                                  | 23        |

|   |           |
|---|-----------|
| <b>SURA YA NNE .....</b>  | <b>24</b> |
| <b>UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....</b>   | <b>24</b> |
| 4.1 Utangulizi wa sura ya nne .....   | 24        |
| 4.2 Kubainisha Tafsida Zinazotumika Katika Lahaja ya Kipemba .....                                  | 24        |
| 4.2.1 Tafsida zinazotumika Msibani .....  | 25        |
| 4.2.2 Tafsida zinazotumika Harusin.....   | 26        |
| 4.2.3 Tafsida zinazotumika Nyumbani .....   | 27        |
| 4.2.4 Tafsida Zinazozungumzwa Kazini.....   | 29        |
| 4.3 Kupambanuwa matumizi ya Tafsida zinazotumika katika<br>Lahaja ya Kipemba .....                  | 29        |
| 4.3.1 Matumizi ya Tafsida katika Mazingira ya Harusini.....   | 30        |
| 4.3.2 Matumizi ya aTuria katika Mazingira ya Nyumbani .....   | 33        |
| 4.3.3 Matumizi ya Tafsida katika Mazingira ya Msibani .....   | 37        |
| 4.3.4 Matumizi ya Tafsida katika Mazingira ya Kazi .....  | 38        |
| 4.4 Kuelezea Faida na Hasara ya Matumizi ya Tafsida katika Jamii Hususani<br>Jamii ya Wapemba ..... | 38        |
| 4.4.1 Faida ya Matumizi ya Tafsida katika Jamii .....   | 39        |
| 4.4.2 Hasara ya Matumzi ya Tafsida katika Jamii .....   | 40        |
| 4.5 Hitimisho.....  | 41        |
| <b>SURA YA TANO .....</b>   | <b>42</b> |
| <b>MUHTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>   | <b>42</b> |
| 5.1 Utangulizi .....  | 42        |
| 5.2 Muhtasari wa Utafiti .....  | 42        |
| 5.2.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti.....  | 43        |

|  |           |
|--|-----------|
| 5.2.1.1 Lengo la Kwanza.....             | 43        |
| 5.2.1.2 Lengo la Pili .....              | 43        |
| 5.2.1.3 Lengo la Tatu .....              | 44        |
| 5.3 Mapendekezo .....                    | 44        |
| 5.3.1 Mapendekezo ya Jumla .....         | 44        |
| 5.3.2 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo ..... | 45        |
| 5.4 Hitimisho.....                       | 46        |
| <b>MAREJELEO .....</b>                   | <b>48</b> |
| <b>VIAMBATANISHI .....</b>               | <b>51</b> |

## ORODHA YA VIAMBATANISHI

|                        |   |    |
|------------------------|---|----|
| Kiambatanishi Na. I:   | Mwongozo wa Maswali ya Hojaji .....   | 51 |
| Kiambatanishi Na. II:  | Usaili Kwa Watafitiwa Ambao Hawajui Kusoma na<br>Kuandika .....   | 54 |
| Kiambatanishi Na. III: | Kinaonyesha Orodha ya Tafsida na Maana Zake .....   | 55 |
| Kiambatanishi Na. IV:  | Kinaonyesha Kisiwa cha Pemba Katika Eneo la Mkoa<br>wa Kusini Pemba .....   | 57 |
| Kiambatanishi Na. V:   | Kinaonyesha Eneo la Chake Chake Mjini Kisiwani<br>Pemba.....  | 58 |
| Kiambatanishi Na. VI:  | Kinaonyesha Kisiwa cha Pemba Ambapo Lahaja ya<br>Kipemba Inazungumzwa .....   | 59 |
| Kiambatanishi Na. VII: | Kinaonyesha Shughuli Mbalimbali za Wananchi katika<br>Eneo la Mjini Chakechake Pemba Ambapo Eneo Hili<br>Ndilo Mtafiti alifanya Utafiti wake Kuwakilisha<br>Pemba Nzima ..... | 60 |

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI WA JUMLA**

#### **1.1 Utangulizi**

Utafiti huu umehusu “kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba”, ambapo umelenga kuchunguza mambo makuu matatu. Kwanza, kubaini kuwepo kwa tafsida mbali mbali zinazotumika katika lahaja ya kipemba. Pili, kuelezea matumizi yake katika jamii ya Wapemba. Tatu, kueleza faida na hasara zake katika jamii ya Wapemba. Surahii pia inatoa taarifa za awali kuhusu mada ya utafiti ambapo mtafiti ataelezea kuhusu usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti yakiambatana na mswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti mipaka ya utafiti hatimae hitimisho, haya yote yameelezwa juu ya kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba.

#### **1.2 Usuli wa Mada**

Wapemba kupitia maisha yao hutumia tafsida kama nyenzo ya kunusuru mazungumzo yao. Katika lugha ya Kiswahili hasa ya kifasihi maneno ya stasha huitwa tafsida. Wataalamu wengi wameelezea kuhusu tamathali za semi ambapo ndani yake inapatikanatafsida. Hivyo Wapemba kupitia lahaja yao ya Kipemba hawakuwa nyuma katika kutumia tafsida ili kunusuru mazungumzo yao. Wataalamu kama vile Jilala (2016), Wamitila (2003), Senkoro (1982), Masebo (2004) na wengine wamefasili dhana ya tafsida kama ifuatavyo:

Senkoro (1982) amesema kuwa “Tafsida hujitokeza kwa utumizi wa maneno, msemu na nahau ambayo hupunguza ukali au matusi badala ya kutumia neno, msemu au nahau kali ama ya kimatusi”, pia ameeleza dhana hii kwa kutilia mkazo wa kuonesha

mifano kama vile, “Kujisaidia au kwenda haja badala ya kunya au kukojoa. Gibbe (1980) ameeleza kuwa ni tamathali ambayo husema mambo kwa lugha laini inayoambaa kuchoma na kutonesha hisia za watu. Mfano siku hiyo ya safari, kujiwa na wito huo, mtu hana hiari wala uwezo.....”

Allan na Burridge (1991) wamesema kwamba nenotafsida limetokana na tafsiri ya “*euphemism*” hutokana na uambatanishi wa viambajengo vya kigiriki “*eu*” kumaanisha “*nzuri*” na “*pheme*” kumaanisha *kuzungumza*. Kwa hivyo neno tafsida kwa tafsiri ya “*eupheme*” kumaanisha kuzungumza kwa maneno mazuri au kuzungumza kwa usemi usioudhi na kudhuru mtu.

Gatambuki (2009) akirejelea mawazo ya Bright (1985) na Allah na Burridge (1991) anaeleza kuwa “tafsida ni kutumia maneno mazuri, matamu, yanayopendeza, yaliyotiwa nakshi yakavutia”, Pia anasema ni kutokusema maneno moja kwa moja ili kuepuka kudhuru uso wa msikilizaji.

Harry (1954) anasema kwamba “lugha huashiria mfumo jamii husika, na kwa hivyo kuna uhusiano wa lugha na jamii ambapo lugha hiyo hutumika. Katika jamii kuna namna lugha inavyotumiwa na kuleta aibu ama hata kuwa ni vigumu kuyatumia maneno fulani katika lugha kuwa ni mwiko. Kwa sababu hii watumizi lugha huweza kukwepa hali hiyo kwa kutumia lugha inayoonekana nzuri au yenye adabu nayo huitwa tafsida. Hivyo basi kwa kuzingatia tafsiri ya Harry (keshatajwa), tunaweza kusema kuwatafsida ni maneno yenye adabu.”

TUKI (1990), wamesema kuwa “Tafsida au ufasidi ni matumizi ya maneno ya staha badala ya yale halisi. Kwa mfano *aga dunia* ni neno la staha na lenye upole linalotumika badala ya *kufa*”

Kutokana na maelezo hayo tunaweza kusematafsida ni maneno yanayoundwa na kila jamii ili kurahisisha mawasiliano, kuyafanikisha na pia kuficha uso wa wanaowasiliana. Kwa ujumla tafsida ni maneno ya heshima ambayo hutumika ili kupunguza ukali wa jambo linalosemwa ambalo aghalabu huwa aibu kutamka mbele za watu au ni karaha. Mfano kusema *sehemu za siri* (uchi). *Kubaua*, (kukojoa), *yuko uani/msalani* (Yuko chooni), *Amechafua hewa* (amejamba), n.k.tafsida hizi na nyingine hutumika ili kunusuru mazungumzo.

TUKI (2004), imeeleza lahaja ni tofauti kati ya matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbali mbali kwa lugha yenye asili moja. Lahaja ya kipemba ni lahaja ya Kiswahili iliyozungumzwa kisiwa cha Pemba isipokuwa eneo la Kusini la Kisiwa hicho ambako yasemekana kunazungumzwa lahaja ya kitumbatu Bakari (2015). Kipemba ni lahaja ya Kiswahili iliyowekwa na Winaisimu katika kundi la kwanza la lahaja za kusini, ambazo eneo lake ni Kenya kusini ukanda wa Mrima, kisiwa cha Pemba na Unguja, lahaja zinazohusika na kundi hili ni kimtang'ata (Kimrima), Kingome (Kimafia/Kingao), kimwani, Kitumbatu, kimakunduchi (Kikae) na kipemba. Lahaja ya kipemba huzungumzwa katika maeneo mbali mbali ya kisiwa cha Pemba ambapo kisiwa hicho kimejigawa katika miji mikuu minne ambayo ni Mkoani, Chake chake, Wete na Micheweni. Mkoani na Chake Chake ipo kusini, Micheni na Wete ipo kaskazini mwa kisiwa hicho, pia Pemba imezungukwa na visiwa vidogo vidogo kama vile Kojani, Fundo, Kisiwa Panza, Makoongwe nk. Maeneo haya yote yanazungumza lahaja ya kipemba, BAIKZA (2012).

Utafiri huu umechunguzamatumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba, ambapo kila jamii ina mfumo wake wa maisha ambao husababisha lugha kutofautiana. Utofauti



ambao husababishwa na mambo mengi yakiwemo utamaduni, lugha, mazingira na hata shughuli zakimaisha kama vile biashara, kilimo, uvuvi n.k.

Kwa kuwa tafsida nimoja kati ya vipengele vya tamathali za semi hivyo basi ipo haja ya kujua ni nini tamathali za semi “Tamathali za semi ni vifananishi au viwakilishi vya dhana moja kwa dhana nyingine zinazofanana Jilala (2016). Mtafiti baada ya kupitia mandiko tofauti aliona maelezo yanayozungumzia tafsida katika muktadha mwingine kama vile maana na mifano ya tafsida, ila hakupata kuona maelezo yaliyoelezea tafsida za lahaja ya kipemba. Hivyo basi utafiti huu umeshughulikia zaidi na kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Hakuna shaka ipo tofauti ya mazungumzo katika kuwasiliana. Mazungumzo hayo huletaugumu wa kutamka na badala yake kutumika maneo ya busara katika kufanikisha mazungumzo. Kutokana na hilo Mtafiti ameona ipo haja ya kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba ambapo matumizi ya maneno kama haya huwafanya wazungumzaji kuyafunika maneno kwa kutumia maneno ya tafsida yenye upole.

Jambo hili ni muhimu hasa katika juhudi ambazo kila jamii hutumia ili kustawaisha na kukuza misingi ya maadili katika maisha ya binaadamu na kutoa mwanga kwa wageni wa lugha ambapo tafsida huzungumzwa kupitia rika (vijana au wazee), mahali (harusini, msibaniau nyumbani), hali (malezi, mafundisho, huzunia hata fura) na kufanikisha mawasiliano. Lakini pia Wataalamu waliowengi hawakuelezea tafsida katika lahaja ya Kipemba, na wameelezea tafsida kama dhana tu kama vile Senkoro,

Masebo, Gibbe, Allan na Burridge (wameshatajwa). Wengine kama vile Mukaria (2011) ameeleza tafsida katika lugha ya Kiimenti na Nguti (2013) ameeleza tafsida katika lahaja ya Kikamba.

Nae Saidi (1976) akizungumzia mazungumzo ya wanawake nanukuu “Hukai ukasubiri *riziki* yako... Mimi mama yako umeniona hivi, *nimevunja ungo* nikakaa kwetu siku zakukaa .... Ameeleza jinsi maneno ya busara yanavyotumika kwa kina mama wanapokuwa wanatoa malezi kwa watoto wao. Mfano *bado mbichi* (Hakongi) *ameaga dunia* (kufa) n.k.

Gibe (1980) ameeleza jinsi tafsida zinavyotumika kutamka mambo kwa kutumia lugha laini isiyochoma hisia za watu. Hivyo, amesena maneno yenye kupunguza ukali wahisia ni bora kutumika katika mazungumzo. Hivyo, mtafiti ameona ipo haja ya kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba na kuwapa mwanga wale wote wasiojua matumizi ya tafsida hizo.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Malengo ya utafiti huu yamegawika katika makundi mawili nayo ni lengo kuu na malengo mahsusi.

##### **1.4.1 Lengo Kuu**

Lengo la utafiti huunikuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba katika jamii ya Wapemba.

##### **1.4.2 Malengo Mahasusi**

Malengo mahsusi katika utafiti huu ni haya yafuatayo:

- (i) Kubainishatafsida zinazotumika katika lahaja ya Kipemba kwa maandishi.
- (ii) Kupambanua matumzi ya tafsida zinazotumika katika lahaja ya Kipemba .
- (iii) Kuelezea faida na hasara ya matumizi ya tafsida hizo katika jamii ya Wapemba.

### **1.5 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu unajibu maswali yafuatayo

- (i) Ni tafsida zipi zinazotumika katika lahaja ya Kipemba?
- (ii) Ni yepi matumizi ya tafsida hizo?
- (iii) Je, tafsida zina hasara na faida gani katika jamii?

### **1.6 Umuhimu wa Utafiti Huu**

Utafiti huu una umuhimu ufuatao:

Kwanza, kutoa mwanga kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili kuweza kuelewa utajiri wa kiswahili na lahaja zake katika kuelezea kile kilichokusudiwa kupitia tafsida za lahaja ya kipemba.

Pia, kuwapa hamasa waandishi wa vitabu na makala waweze kuandika maneno ambayo yataleta heshima na kuonesha busara katika uandishi wao. Vilevile, Utafiti huu utatumika kama marejeo kwa watunzi na waandishi wa Makamusi.

Kwa kuongea utafiti huu utasaidia katika kukuza maadili ya jamii ili kuimarisha maisha ya jamii na kujenga ubinaadamu. Mwisho, kutoa uelewa kwa wanajamii wengine katika kuelewa vyema lahaja ya kipemba na kuongeza utajiri wa msamiati wa lahaja ya kipemba.

### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umekusudia kuchunguza matumizi yatafsida katika lahaja ya kipemba. Katia kufanya hivi utafiti huu uliamua kuchunguza tafsida katika eneo dogo linalowakilisha eneo lote la Pemba, eneo hilo ni Chake Chake mjini ambapo ni eneo linalojumuisha Wapemba kutoka Kusini na Kaskazini mwa Kisiwa cha Pemba, kwa shughuli zao tofauti za kujitafutia maisha yao, shughuli hizo kama vile wafanyabiashara, wafanya kazi, wasafiri na wasafirishaji n.k. ambao hutumia tafsida wanapokuwa katika maeneo yao wanakotoka pia katika shughuli zao wanazofanya.

### **1.8 Hitimisho**

Sehemu hii ilianza na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti lengo kuu na malengo mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na hatimae mipaka ya utafiti ambapo ilitoa fursa ya kuanza kwa sura ya pili.

## **SEHEMU YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Sura hii imehusu utalii (mapitio) tofauti ya dhana na kazi tangulizi kuhusu mada pamoja na mkabala wa kinadhari uliotumika katika utafiti huu.

#### **2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi**

Kipengele hiki kitafafanua dhana ya tamathali za semi, tafsida lahaja pamoja na kazi tangulizi kuhusu tamathali za semi, tafsida na kazi tangulizi kuhusu lahaja za Kiswahili.

##### **2.2.1 Dhana ya Tamathali za Semi**

Dhana ya tamathali za semi imefafanuliwa na wataalamu mbali mbali kama ifuatavyo: Senkoro (1952):” Tamadhali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusoma” anaendelea kusema “wakati mwingine hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha” pia amezianisha kuwa ni tashbiha, tashhisi, sitiari, kijembe, kejeli, tafsida na nyinginezo. fasili hii inatupa uelewa katika utafiti huu wa kujua kuwa tamathali za semi hupelekea kuipamba lugha na kuifanyaiete ladha katika mazungumzo, kama vile ambavyo tafsida inaipamba lugha na kuimarisha mazungumzo.

Mulokozi na Kahigi (1979) Wamesema “Tamathali za semi ni vifananishi au viwakilishi vya dhana moja kwa dhana ya pili tofauti zinazofanana. Ni usemi wenye

kupanua, kupunguza au kubadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalum ya kishairi iliyokusudiwa.”Kwa kuzingatia maana hiyo ya Mulokozi na Madumulla (wametajwa) Mtafiti aliweza kupata msingi wa uelewa kuwa tamathali za semi ni usemi maaluma ambao huimarisha na kupanua maana ya jambo. Mtafiti alitumia muongozo huo wakati wa kuchambua faida na hasara za tafsida.

Wafula (2003) anaeleza” tamathali za semi ni maneno yenye kurejelea maana iliyofichwa.” Kwa maana hii iliyoelezwa na Wafula (ameshatajwa) mtafiti aliweza kuchunguza tafsida kama kipengele cha tamathali za semi, hasa tafsida zinazozungumzwa na jamii ya Wapemba na kuzibainisha katika makundi mbali mbali.

Wamitila (2003) amesema “Tamathali ya (za) semi hutumiwa kuelezea fungu la maneno au hata ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine”. Yeye ameeleza kuwa tamathali za semi hueleza fungu la neno au maneno yaliyogeuzwa maana yake, Kwa kuwa mtafiti amechunguza *Matumizi ya Tafsida Katika Lahaja ya Kipemba*, maana ya Wamitila (ametajwa) imemuongoza mtafiti kufafanua maana mbalimbali kama zinavyoonekana katika uchambuzi wa data za utafiti huu.

Madumulla (2009), anasema “Tamathali za semi ni fungu la maneno linalogeuzwa maana yake kamili ili kuwakilisha maana nyigine. Mfano subira ni nguo njema nayo kwa hiyo jitande.”Maana hii iliyoelezwa na Madumulla (keshatajwa) inatupa uelewa kuwa ni maneno yenye maana maalumu. Hivyo, itamuongoza mtafiti katika kupata na kuchagua tamathali za semi.

John na Mduda (2012) Wameelza “Tamathali za semi ni misemo ambayo hutumiwa kutoa maana tofautina maana ya maneno yake “Katika maana hii imelezwa kuwa ni kutoa maana toauti na maana nyingine ambapo tafsida pia ina sifa ya kutumia neno kukusudia maana nyingine. Kwa kigezo cha maana hii kimemuongoza mtafiti katika uchambuzi wa data za utafiti hasa katika kipengele cha faida na hasara za tafsida.

Jilala (2016) ameeleza “Tamathali za semi ni vifananishi au viwakilishi vya dhana nyingine tofauti au zinazofanana nazo ambazo hutumiwa kwa lengo la kupanua, kupunguza, kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida ili kuwasilisha ujumbe na maana iliyokusudiwa kwa hadhira” Ameeleza kuwa “huweza kutumika katika vilinganishi kwa kazi za fasihi zilivyotumika katika kazi moja au nyingine”. Katika kazi yake ameeleza tamathali za semi, lakini pia amezitaja kama vile Tashbiha, Tashhisi, Taashira, Ishara, Takriri, Sitiari ila hakuelezea tafsida ambapo ni moja kati ya tamathali za semi. Maana hii imetupa muelekeo katika utafiti huu kuona kuwa tafsida ni moja kati ya tamathali za semi inayotumia vifananishi vya dhana moja kwa lengo la kubadilisha maana nyingine kama ilivyoonekana katika matumizi ya taria. Kwa hivyo, utafiti huu utaelezea *Kuchunguza Matumizi ya Tafsida Katika Lahaja ya Kipemba*.

### **2.2.2 Dhana yaTafsida**

Dhana ya tafsidaimeelezwa na Wanaisimu kwa njia tofauti, kwa mfano:

Kuhenga (1977) ameeleza kuwa tamathali za semi ni nguzo za ufasaha na mapambano ya lugha na humuwezesha mdadisi wa lugha kupakuwa baadhi ya uhondo uliofichika katika lugha. Mawazo yake yamesaidia mtafiti katika kuona ni jinsi gani tunaweza kuchambua matumizi ya tafsida zinazojibainisha katika jamii.

Senkoro (1982) amesema “Tafsida hii hujitokeza kwa utumizi wa neno, msemu na nahau ambao hupunguza ukali wa matusi badala ya kutumia neno, msemu au nahau kali ama ya kimatusi” Senkoro (ameshatja) maelezo dhana hii kwa kutilia mkazo kwa kuonesha mifano kama vile; *kujisaidia* na *kwendahaja* badala ya kunya au kukojoa.

Fromkin na Rodman (1988:189) wanasema kwamba,” jamii katika hali yake ya uvumbuzi wa lugha hubuni maneno na kisha huamua nini chafaa kuzungumzwa kwa upole na nini hakifai. Wanadai kwamba maneno yote yako wazi kwa mzungumzaji ili ayatumie lakini muktadha wa jamii hauna kile kinachosemwa na kisemwe wapi na lini”. Wanaendelea kusema, “uchafu na urembo wa lugha hutambulika katika sikio la msikilizaji au sikio la jamii nzima”. Kutokana na ufafanuzi huo, utafiti huu utafaa kile kilichoandikwa na Wataalamu hawa kwani kina umuhimu mkubwa kwa sababu mawazo yaliyomo katika dhana hizi tumeyatumia katika kufafanua maana za tafsida mbalimbali, jambo ambalo lilipelekea kufikia malengo ya utafiti wetu uliokusudia kuchunugza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba.

Msokile na Madumula (1991) Wamesema, “Tuaria ni tamathali ya usemi yenye heshima kwa kuwa hujaribu kumpa mtu heshima yake” Masebo na Nyangwine (2004) wamesema “Ni kupunguza ukali wa maneno au matusi katika usemi” BAKIZA (2010) imesema,” Tafsida ni tamathali ya semi inayotumika kuficha karaha au matusi”.

Kutokana na ufafanuzi huo, utafiti huu utafaa kile kilichoandikwa na Wataalamu hawa kwani kina umuhimu mkubwa kwa sababu mawazo yaliyomo katika dhana hizi tumeyatumia katika kufafanua maana za tafsida mbalimbali, jambo ambalo lilipelekea



kufikia malengo ya utafiti wetu uliokusudia kuchunugza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba.

### **2.2.3 Dhana ya Lahaja**

Lahaja ni dhana ambayo imejadiliwa na wataalamu mbalimbali kwa mitazamo tofauti, yafuatayo ni mawazo ya dhana ya lahaja kupitia wataalamu tofauti. Ngugi na Chacha (2004:37). Lahaja ni aina ya uzungumzaji unaotumiwa na kikundi cha watu aghalabukatika eneo maalumu, na hutofautiana uzungumzaji na vikundi vingine vya lahaja hiyo moja katika matamshi, msamiati na kwa nadra sarufi.

Mdee (2014) anafasili lahaja kuwa ni kilugha kimojawapo cha lugha, ambacho hutofautiana na vilugha vingine kutokana na wazungumzaji wake kuhama na kuishi mbali na wingine na kutenganishwa na maumbile ya asili kama vile milima, mito na bahari mabonde na kadhalika. TUKI (2004) imeeleza, Lahaja ni tofauti kati ya matamshi, maumbo na matumizi ya manenokatika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja.

Fasili zote hizo ni sahihi kwani zimetaja mambo muhimu kama vile utofauti wa kifonolojia, kimsamiatina lafudhi. Tofauti za kimsamiati na kimatamshi ni kubwa zaidikiasi kwamba wakati mwingine mawasiliano na watu wa lahaja tofauti yaweza yakakwama. Kwa hiyo utafiti huu kwa kuzingatia dhana hiyo yalahaja utaangalia matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba.

### **2.4.4 Kazi Tangulizi Kuhusu Tafsida**

Awali mtafiti amesema kuwa tafsida zimefanyiwa utafitina wataalamu wengi, miongoni mwao nihawa wafuatao:

(Hymes 1964) Kwa kumnukuu Nadel (1954), na pia Wardhaugh (2002) wamewataja Wanupe wa Afrika Magharibi kama mojawapo ya watu wapole ulimwenguni kwa kufanya uteuzi muwafaka wa maneno yanayofaa zaidi na yasiyofaa katika mazungumzo. Wao huamua kutumia tafsida moja kwa moja ili kutaja sehemu nyeti za mwili”. Kazi hii imetupa mwanya wa kutaka kuona faida na hasara za tafsida zinazotumika katika lahaja ya Wapemba katika mazungumzo yao kwa kule kuteua maneno yanayofaa na yasiyofaa katika mazungumzo.

Kazi ya Njeri (2007) alichunguza tafsida katika mazungumzo kuhusu virusi vya UKIMWI na kusema kwamba” kuna wakati ambapo tafsida hukwamisha mawasiliano hasa pale ambapo pana uana, umri, hata kazi wazifanyazo wazungumzaji na wasikilizaji. Anasema ingawatafsida hutumiwa kama mikakati ya kupunguza athari hasi baadhi ya hizo zina athari za uso bado”. Utafiti huu ulitufaa kwani unaonyesha matumizi yatafsida katika lugha ya Kikuyu katika hali tofauti ya ugonjwa wa Ukimwi, utakuwa tofauti na utafiti wetu ambao unachunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba, hivyo tulitumia mawazo hayo katika kuimarisha kazi yetu na kufikia malengo ya utafiti wetu.

Kazi ya Wambua (2009) alitafiti kuhusu tofauti ya matumizi ya kilahaja na mitazamo ya kileksika za miiko na tafsida katika jamii ya Kikamba. Katika utafiti wake aliweza kutofautisha jinsi mitazamo tofauti inavyojitokeza katika matumizi na maana ya leksika za miiko na tafsida kwa kulinganisha lahaja za lugha ya Kikamba. Ingawa utafiti huu ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu umeshughulikia miiko na tafsida, hata hivyo umetufaa kwa kuwa umeshughulikia tafsida katika jamii ya Kikamba na sisi tunashughulikia matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba.

Mukaria (2011) anazungumzia aina tofauti za tafsida alizoandika kuhusu maneno ya miiko na tafsida katika lahaja ya Kiimenti. Kazi hii imetufaa kwa sababu imezianisha tuaria katika makundi tofauti ya miiko na utafiti huu unahusu matumizi ya tafsida katik alahaja ya Kipemba. Kwa msingi huo utafiti wa Mukaria (keshatajwa) kama nyezo kuu ya kuu ya kuainisha tafsida katika jamii ya Wapemba. na kutupeleka mbele zaidi kuona jinsi tafsidadinvyoweza kuibua faida na hasara katika matabaka ya watu kimatumizi.

Kazi ya Nguti Mary (2013) imechunguzatafsida kwa kulinganisha tafsida ya lugha ya Kikamba na Kiswahili, katika utafiti wake huo unafikia hitimisho kuwa tafsida hizi huundwa na watumizi lugha wa tafsiri na watumizi lugha wa jamii yenye utamaduni mmoja. Tafsida hizi huundwa kwa njia moja wapo ya kuelezamambo au kusema jambo kwa njia ya kutumia maneno au lugha kwa upole na adabu ili kuficha mambo yanayoonekana mabaya au yanayoibisha na kudunisha. Utafiti wa Nguti (keshatajwa) ulikuwa ni msaada mkubwa kwa mtafiti kwa sababu ulimuongoza katika kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba wakati wa uchambuzi wa data za utafiti.

### **2.2.5 KaziTangulizi Kuhusu Tamathali za Semi**

Ni dhahiri kwamba tafsida ni moja ya kipengele kiacho patikana katika tamathali za semi, hivyo ipo haja ya kuona kazi ambazo zilifanywa kupitia wataalamu na watafiti tofauti kama ifutavyo. Nae Khatibu (1986) ameeleza kuwa tamathali za semi zinazotumika katika tanzu mbali mbali za fasihi kama vile riwaya, tamthiliya, ushairi, hadithi fupi na fasihi simulizi. Tamathali za semi alizotaja ni pamoja na tashibha, tashhisi, sitiari, takriri, simango, kejeli, misemo, taashira, nasihi, tanakali sauti, chuku na ritifaa. Uainishaji huu wa tamathali za semi uliofanywa na Khatibu (keshatajwa)

ulikuwa ni msaada mkubwa kwetu,hasa ukizingatia utafiti huu pia katika lengo lake moja ni kubainisha tafsida zinazopatikana katika lahaja ya kipemba.Hivyo mawazo yake yalitumika katika kufikia lengo la utafiti huu.

Aidha, Mlacha (1989), amefanya utafiti juu ya matumizi ya sitiari katika *Riwaya ya Rosa Mistikana* kufanikiwa kuibua sitiari za aina tofauti. Katika utafiti wake aliweza kubainisha maana na matumizi ya sitiari mbalimbali zilizojitikeza katika riwaya teule. Kwa sababu kazi ya fasihi huwakilisha jamii ya watu husika,kwa mnasaba huu mtafiti alipata mwanga kupitia uchunguzi uliofanywa na kuweza kuhusisha na jinsi tafsida zinavyotumiwa na jamii ya Wapemba na kufikia lengo lililokusudiwa.

Kazi ya Mjema (1990) amefanya utafiti juu ya matumizi ya lugha na dhamira katika *Riwaya ya Kusaidika*. Katika uchunguzi huo, alibaini kwamba mtunzi wa *Riwaya ya Kusaidika* imetumia matumizi ya lugha ya kejeli, mafumbo na kebehi. Matumizi ya kebehi yaliyojitokeza katika *Riwaya ya Kusaidika* ni kule kutumia mandhari ya nchi inayoelea angani lakini mambo yanayofanyika katika nchi hiyo ni yale yanayotokea katika ulimwengu wa kawaida. Hivyo uchunguzi wa Mjema (ameshatajwa) umetusaidia katika utafiti huu kwani umepelekea kuchunguza tafsida kama ni miongoni mwa tamathali za semi kwa kuchunguza matumizi yake katika lahaja ya kipemba.

Khamis (2007), alichunguza mitindo mipya katika uandishi wa *Riwaya ya Kiswahili ya kisasa* Khamis (ameshatajwa) ameeleza kuwa matumizi ya lugha ya tamathali za usemi yanajitokeza pia katika riwaya za kisasa zikiwa na sifa ile ileya uhalisia ajabu na uhalisia mazingaombwe. Mawazo ya Khamis (ameshatajwa) yametusaidia katika kufanikisha utafiti huu kwa kuchunguza tafsida katika lahaja ya kipemba.

Kazi ya Mussa (2015), imeeleza tamathali za semi jinsi zinavyoibua dhamira katika Tamthilia ya Ulinganishi wa *Morani* na *Funuo Liongo*. Katika utafiti wake amegundua kwamba mfanano mkubwa wa tamadhali za semi katika uibuaji wa dhamira umejitokeza katika tamathali ya sitiari kuliko tamathali nyingine kama vile tashibiha, takriri na tashhisi. Utafiti wa Mussa ulitusukuma kupata msingi wa kubaini maana zilizomo katika tafsida na namna zinavyotumika na kutufikisha katika malengo yetu.

Maryam (2016), nae alitafiti matumizi ya tamathali za semi katika *Riwaya ya Haini* katika utafiti wake alibaini kuwa tamathali za semi hutumiwa na Waandishi wa kazi za fasihi na zina nafasi kubwa sana katika kuibua dhamira katika kazi yoyote ya kifasihi na hatimae kufikisha ujumbe katika jamii. Kupitia kazi hiyo mtafiti alipata nafasi ya kuchambua matumizi ya tafsida na kuona yanaleta faida gani katika jamii ya Wapemba.

## **2.2.6 Kazi Tangulizi Kuhusu Lahaja za Kiswahili**

Wataalamu mbalimbali walijitokeza kuchunguza baadhi ya lahaja za Kiswahili. Kwa mujibu wa Kipacha (2004) kazi ya mwanzo ya utafiti wa lahaja za kiswahili iliandikwa mwanzoni mwa karne ya 19 ili kufahamu lugha za wenyeji wa pwani na kurahisisha shughuli za uwenezi wa dini na utawala. Lahaja kadhaa zimechunguzwa kama vile Kimtang'ata (Whiteley, 1956), Chichifundi (Lambert, 1958) na Kipemba (Whitely, 1958). Mwishoni mwa karne ya 20 walijitokeza Wanalugha wazawa kuchunguza lahaja za Kiswahili kuendeleza kazi zilizofanywa na watafiti Wageni. Batibo (1982), Khamisi (1984) na Mshindo (1989) ni miongoni mwa waliofanya tafiti za lahaja za Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya wataalamu hao wamejikita katika

kuchunguza vipengele vya sarufiza lahaja hizo wakilinganisha na vile vya Kiswahili sanifu. Kwa kuptia kazi walizofanya wataalamu hao Mtafiti alipata msukumo wa kuchunguza lahaja ya Kipemba kupitia matumizi ya tafsida za lahaja ya Wapemba.

### **2.3 Pengo la Utafiti**

Tafiti nyingi ambazo mtafiti alizipitia, Mtafiti kama vile Mukaria (2011), Njeri (2007), Nguti (2013), Khatibu (1986), Kuhenga (1977) n.k. tumeona kuwa zimelezea dhana ya tafsida ila hawakueleza tafsida katika lahaja ya Kipemba. Kutokana na hali hiyo, mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti wa kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba.

### **2.4 Mkabala wa Nadharia**

Kazi yeyote inayofanyiwa utafiti ni lazima iwe imehusishwa na nadharia ambayo inahusiana na kazi hiyo. Hivyo ipo haja kwa utafiti huu kuelezea kwa kina maana ya nadharia na kuonesha ni nadharia ipi itatumika katika utafiti huu.

#### **2.4.2 Nadharia ya Simiotiki**

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) ”*Simiotiki* ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara au uashiraji wa jambo”. Muasisi wa nadharia hii ni Fredinand Dissausare katika miaka ya 1970 anasema, katika matumizi ya lugha kuna vitu viwili kitajwa na kitaja. Mara nyingi hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitajwa na kitaja, hii ndio inayopelekea kitu kimoja kiweze kuitwa majina tofauti. Nadharia hii inatufahamisha juu ya kufahamu matumizi ya lugha ya ishara kuwa yanarejelea nini katika kazi ya fasihi. *Nadharia ya Simiotiki* inajihusisha na ufumbuzi na ufumbuaji wa mafumbo katika kazi ya fasihi. Nadharia hii ina misimbo mitano nayo ni msimbo wa kimatukio, kihementiki, kiurejelezi, kiseme na kiutamaduni. Katika nadharia hii suala

la ishara na uashiriaji ni muhimu katika kuangalia kazi ya kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba. Katika utafiti huu Mtafiti alitumia msimbo wa kiurejelezi ambao hutumia maneno yenye kurejelea mambo mbalimbali yenye uhusiano fulani na maneno yenyewe.

Mapungufu ya nadharia hiini kuwa inachukulia ishara zote kila mahali na kila wakati zina maana, inapuuza hali ambapo ishara zingine ambazo hazijabeba ujumbe wowote. Griffen (1997:118) amesema “ni kweli kuwa, Simiotiki ni hatari ya kuwa kila kitu kinapewa ishara kiasi cha kupoteza uhalisia” kwa hiyo nadharia hii licha ya kuwa inaudhaifu huo lakini bado ina mashiko makubwa katika kazi hii inayochunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba, kwa sababu inakusudia kufikisha ujumbe wa kile kilichoashiriwa katika tafsida za lahaja ya kipemba.

Sababu ya kuchagua nadharia hii ni kwamba, ni nadharia ambayo inafaa kutuongoza katika utafiti huuhasakatika ufafanuzi wa ishara zilizobebwa na tafsida. Hivyo basi nadharia ya simiotikiitatumiwa na mtafiti katika uchambuzi wa lugha ya ishara na mafumbo yaliyomo katika tafsida za kipemba, jambo ambalo limesaidia kufikia malengo ya utafiti wetu.

## **2.5 Hitimisho**

Sura hii imejadili dhana na mapitio ya kazi tangulizi yanayohusu mada pamoja na kiunzi cha nadharia, katika mapitio ya kazi mtafiti hakupata kuona kazi yoyote iliyozungumzia kuhusu matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba. Hivyo utafiti huu umechunguza kwa kina matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba, ambapo uchunguzi huo utaongozwa na nadhariaya Simiotiki ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Sura inayofuata ni sura ya tatu.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii imejadili kwa kina hatua, njia na mbinu mbali mbali zilizotumikakatika ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti, wenye lengo la kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba. Pia sura hii imeeleza vipengele mbali mbali kama vile eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu zilizotumika katika kukusanya data, vifaa vilivyotumika kukusanyia data, kundi lengwa la utafiti pamoja na mbinu za uchambuzi wa data.

#### **3.2 Eneo la Utafiti**

Kothari (2004) eneo la utafiti “ ni eneo ambalo mtafiti huliteuwa kwa ajili ya kufanyia utafiti wake ili kumuwezesha kutimiza malengo yake” . Eneo hili huteuliwa kwa kuzingatia upatikanaji wa data na sababu za kimazingira kwamba ni eneo ambalo linaweza kufikika kwa urahisi. Katika kuteua eneo, mtafiti aliamua kuteua eneo la Kisiwa cha Pemba ambako lahaja ya Kipemba inazungumzwa. Kutokana na hilo, mtafiti ameteua eneo la mjini Chake Chake kuwa ni eneo lake la utafiti ambalo ameona limempatia data zatafsida katika lahaja ya Kipemba.

#### **3.3 Mbinu za Kukusanyia Data**

Ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ya utafiti .Ni njia atakayoitumia mtafiti na kuweza kumpatia data zilizo sahihi juu ya utafiti wake.Kothari (1990) anasema “mbinu ya ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambao humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya



utafiti. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu mchanganyiko katika kukusanya data za utafiti. Mbinu hizo ni pamoja na usaili, Uchunguzi Makini, Hojaji na Maktaba. Mbinu hizi mchanganyiko zimetumika ili kupata data zilizo sahihi na kupata matokeo yaliyobora.

### **3.3.1 Usaili**

Njia hii ni njia inayohusisha uwasilishaji wa maswali kwa wasailiwa na kujibiwa kwa njia ya mdomo na mtafiti kuweza kurikodi. Kombo (2006) anasema “Ni majibizano ya ana kwa ana au uso kwa uso, kwa mawasiliano ya simu, barua pepe n.k. yanayofanywa na watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya data” Mtafiti ametumia usaili kwa watafitiwa wake uso kwa uso pamoja na mawasiliano ya simu katika kukusanya data za matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba. Sababu ya kutumia mbinu hii ni kwamba mtafiti alikuwa huru kuelezea kile anachokitafitina kupata data zilizosahihi.

Mtafiti alifanya usaili kwa watafitiwa ambapo alizingatia zaidi wazee na wasiojua kusoma akiongozwa na muongozo wa maswali ya usaili kueleza tafsida zinazotumika katika lahaja hiyo na kupata data zilizo sahihi.

### **3.3.2 Uchunguzi Makini**

“Ni njia ambayo inafanyika kwa kukusanya data inayohusika na kurikodi watu matukio mbali mbali kwa mpangilio maalumu “Williman (2005), Uchunguzi makini ni mbinu ya kukusanyia data inayohusiana na kurikodi tabia za watu, vitu na matukio katika mpangilio maalumu”. Hivyo kupitia mbinu hii mtafiti amehudhuria katika shughuli mbali mbali kama vile harusi, misiba, biashara na hata kushiriki katika mazungumzo ya kawaida ya watu katika jamii. Mbinu hii imemsaidia mtafiti kupata

taarifa zilizo za ukweli na za awali kutoka katika maeneo yaliyotajwa hapo awali ili kutimiza lengo la kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba kwa Wapemba wenyewe.

### **3.3.3 Mbinu ya Hojaji**

Ni njia ambayo mtafiti aliitumia kwa kuandaa maswali yaliyokusudiwa kupata data kwa mtafiti. Kothari (1990) anasema. “Hojaji ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti huandaa maswali yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Mbinu hii inahusu orodha ya maswali na maelezo ya jinsi ya kujibu maswali hayo kwa lengo la kumpatia mtafitiwa majibu.

Mbinu hii ilitumika kwa sababu ya kutoa ufafanuzi mzuri kwa mtafitiwa kuhusiana na mada endapo mtafitiwa atashindwa kulitamka neno kwa kuchelea kuona aibu, pia mbinu hii hutoa uhuru kwa watafitiwa kuelezamawazo yao kwa ubainifu na uwazi na kupelekea kupata taarifa nyingi zaidi. Njia hii iliwahusu zaidi watafitiwa wanaojua kusoma na kuandika kwa kujibu maswali waliyotakiwa kujibu kwa kuandika data zilizosahihi ili kufanikisha utafiti huu.

### **3.3.4 Mbinu ya Maktabani**

Ni mbinu unayohusiana na mapitio ya kazi mbali mbali zilizofanywa na watafiti waliotangulia kuhusiana na mada ya utafiti. Kazi hizo zinawezakuhusu nadharia mbali mbali au hata uchambuzi wa data zinazohusiana na mada ya utafiti husika na maana moja ama nyigine (Kothari 1990). Katika utafiti huu mbinu hii ilitumika kwa kusoma makala, machapisho, kupitia makamusi na vitabu mbali mbali na kupata data zinazotaja tafsida na matumizi yake na kufikia lengo lililokusudia.

### **3.4 Mbinu ya Uchambuziwa Data**

Utafiti huu umetumia mbinu ya maelezo katika kuchanganua data. Enon (1999:24) anasema kuwa “Njia ya maelezo ni njia ya ufafanuzi wa kawaida ambao nambari hazitumiki “yaani ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Kutokana na hilo, Mtafiti alitumia njia ya maelezo katika kuchambua data. Kwa sababu mtafiti anachunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba, hivyo kutokana na uhalisia wa mada hauzingatii idadi ya wazungumzaji na inazingatia mazungumzo, njia ya maelezo ndio ambayo ilihitajika zaidi kuliko ya idadi. Hata hivyo, itakapolazimika kutumia njia ya kiidadi (kitakwimu) mtafiti atatumia.

### **3.5 Usampulishaji**

Best (1996) ameeleza usampulishaji ni njia au utaratibu wa kuteua washiriki kutoka katika kilakundi kubwa jumla la watafitiwa wote”. Utafiti huu uliteua watu wachache miongoni mwa watu wengi waliopo katika jamii ya Wapemba na wanaozungumza lahaja ya kipemba kwa kuzingatia uteuzi wa njia ya unasibu wa kieneo: yaani waliteuliwa kwa njia ya bahati nasibu kwa kuzingatia eneo lililokusudiwa na idadi iliyokusudiwa. Kutokana na hilo wazee 20 na vijana 15 waliteuliwa katika mji wa chake chake Pemba, ili kupata data zinazohusiana natafsida katika lahaja ya Kipemba. Mtafiti alifanya hivyo kwa kuaminikuwa tafsida za kipemba zinapatikana kutoka kwa Wapemba wenyewe.

### **3.6 Sampuli**

Babbie (1999:205) anasema “Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa ambalo limechaguliwa kutoka katika kundi kubwa kwa lengo la kutoa data za kuwakilisha

kundi kubwa. Utafiti huu ulitumia sampuli ya Wazee na vijana. Wazee walikuwa ishirni (20) wakiwemo wanawake kumi (10) na wanaume (10), kwa apande wa vijana ni kumi na tano (15) wakiwa wanawake saba (7) na wanaume nane (8) jumla yao walikuwa watu thelathini na tano (35). Uteuzi huu ulijumuisha wasomi na wasiosoma pia maelezo kwa ufupi yaliwakilishwa na jadweli lifuatalo

| <b>Kundi</b> | <b>Umri</b> | <b>Wanawake</b> | <b>Wanaume</b> | <b>Jumla</b> |
|--------------|-------------|-----------------|----------------|--------------|
| Wazee        | 60-80       | 10              | 10             | 20           |
| Vijana       | 20-50       | 7               | 8              | 15           |

### **3.7 Hitimisho**

Sura hii imefafanua mbinu za utafiti ikiwa pamoja na eneo la utafiti. Mbinu za kukusanyia data nazo ni usaili, uchunguzi makini, mbinu ya hojaji na mbinu ya maktabani. Pia imeeleza zana za kukusanyia data, mbinu za uchambuzi wa data, usampulishaji na sampuli katika kukamilisha utafiti huu.

## SURA YA NNE

### UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

#### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliziwasilisha data zilizokusanywa kutoka katika vyanzo vya data kama vilivyoielezwa katika sura ya tatu. Uchambuzi huu umezingatia mambo matatu. Kwanza mtafiti amewasilisha na kuchambua data zake kwa kuzingatia malengo na maswali ya utafiri aliyoyadhihirisha kwenye kifungu 1.3.2. Jambo la pili, Uwasilishaji na uchambuzi wake umezingatia kiunzi cha nadharia kilichopendekezwa kwenye kifungu 2.4.2. Jambo la tatu mtafiti amewasilisha uchambuzi wa data zilizobainishwa kuwa atazitumia kama alivyozonesha kwenye kifungu 3.5.

Utafiti huu ulitumia nadharaya *Simiotiki* ambayo ilitumika kuchunguza matumizi ya tafsida katikalahaja ya kipemba. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba, ambapo ulikuwa na malengo mahsusi yafuatayo:-

- (i) Kubainisha tafsida zinazotumika katika lahaja ya kipemba.
- (ii) Kupambanua matumizi ya tafsida zinazotumika katika lahaja ya kipemba.
- (iii) Kueleza faida na hasara ya matumizi ya tafsida hizo.

#### 4.2 Kubainisha Tafsida Zinazotumika Katika Lahaja ya Kipemba

Lengo hili liliongozwa swali lisemalo. Ni tafsida zipi zinazotumika katika lahaja ya Kipemba? Suala hili lilijibiwa na watafitiwa thelathini na tano (35) kuptia hojaji na usaili, sawa na asilimia mia moja (100%), ambapo walisema ndio zipo tafsida zinazotumika katikalahaja ya kipemba na hakuna aliyekataa kutokuwepo kwake jumla ya tafsida 68 zilipatikana kwa watafitiwa. Hii ni dhahiri kwamba wapemba hutumia

tafsida katika mazungumzo yao. Hivyo mtafiti baada ya kupata data za tafsida alipata fursa ya kuzibainisha tafsida hizo ambazo zinatumiwa katika mazingira tofauti ya mazungumzo ya Wapemba. Nguti (2013) amegawa tafsida katika mazingira tofauti ya katika shughuli tofauti za Wazungumzaji “Tafsida ambazo hutumiwa katika lugha ya Kikamba na Kiswahili huwa zimetokana na shughuli za kila siku kulingana na muktadha au kundi la Wazungumzaji”. Shughuli ambazo ndani yake huzungumzwa tafsida ni kama vile tafsida katika sherehe na mikutao, matanga, tohara, kazi, wanaume, wananawake n.k. Kupitia utafiti huu mtafiti amezibainisha tafsida katika mazingira ya Msibani, Harusini, Nyumbani na Kazinitafsida ambazo Wapemba wanazitumia kama ifuatavyo:

#### **4.2.1 Tafsida zinazotumiwa Msibani**

Zifuatazo ni tafsida zinazotumiwa msibani kwa lengo la kupunguza majonzi, mshituko wa moyo na hata simanzi kwa watu wanapotokezewa na misiba katika jamii ya Wapemba. Tafsida 9 zilipatika sawa na asilimia 13.23 ya tafsida zilizokusanywa kwa watafitiwa.

| <b>TAFSIDA</b>            | <b>MAANA</b> |
|---------------------------|--------------|
| Faradhi                   | Kifo         |
| Ametangulia mbele ya haki | amekufa      |
| Mavani                    | makaburini   |
| Tusi                      | jeneza       |
| Malaloni                  | amezikwa     |
| Tumepata msiba            | mtu amekufa  |

|                   |                |
|-------------------|----------------|
| Mgonjwa amemaliza | mgojwa amekufa |
| Amehitajika       | amekufa        |
| Amefikia hatma    | amekufa        |

#### **4.2.2 Tafsida zinazotumika Harusin**

Zipo tafsida ambazo hutumiwa katika sherehe mbalimbali za nyumbani ambazo zinawahusu wanajamii, sherehe kama za harusi hutumia maneno yakiwemo ya tafsida ili kuendeleza utamaduni wa jamii katika jamii husika, jumla ya tafsida 16 zilipatikana sawana asilimia 23.52 ya tafsida zilizokusanyawa, zifuatazo ni tafsida zinazotumika harusini.

| <b>TAFSIDA</b>  | <b>MAANA</b>                      |
|-----------------|-----------------------------------|
| Kigozi manyonya | Sehemu ya siri ya mwanamke (uke)  |
| Mtaimbo         | sehemu ya siri ya mwanamme( uume) |
| Kungwi          | mkukufunzi wa harusi              |
| Sharia          | haki ya ndoa                      |
| Kuchukua jiko   | kuoa                              |
| Kuasi ukapera   | kuoa                              |
| Kujitwika       | kuoa                              |
| Anachukua mzigo | anaoa                             |
| Kijiti          | sehemu ya siri ya mwanamme        |
| Mnyumba         | mke au mume                       |
| Wamelala        | wanafanya tendo la ndoa           |
| Wamepumzika     | wanafanya tendo la ndoa           |

|               |                              |
|---------------|------------------------------|
| Somo          | mkufunzi wa mwari( msichana) |
| Jambo         | tendo la ndoa                |
| Kachumbari    | shanga za kiuno              |
| Mvua inayesha | kupata damu ya mwezi         |

#### **4.2.3 Tafsida zinazotumika Nyumbani**

Katika mazingira ya nyumbani tafsida hutumika sana kuliko mazingira mingine,hii ni dhahiri kwamba ustaarabu na upole wa mazungumzo unahitajika zaidi.Tafsida 38zilipatikana sawa na asilimia 55.88 ya tafsida zilizokusanywa, tafida hizo ni kama zifuatazo:

| <b>TAFSIDA</b>   | <b>MAANA</b>                    |
|------------------|---------------------------------|
| Ana wageni       | kupata damu ya mwezi            |
| Mja mzito        | mtu mwenye mimba                |
| Hawajakunana     | hawajafanya tendo la ndoa       |
| Mchafu           | ananatokwa na damu ya mwezi     |
| Yuko kwenye siku | amepata damu ya mwezi           |
| Ukama            | uzi unaofungwa kiunoni          |
| Ng'ande          | uchafu                          |
| Kujifungua       | kuzaa                           |
| Kufundua         | kuota maziwa(machuchu)          |
| Ujusi            | kupata damu baada ya kujifungua |
| Barua            | talaka                          |
| Mwega            | sidiria                         |
| Kufuli           | chupi                           |



|                       |  |
|-----------------------|--|
| Kujisaidia            | kunya au kukojoa   |
| Kutabaali             | kukojoa  |
| Kubaua                | kukojoa  |
| Mkono wa Shati        | mwanaume aliyekosa nguvu za kiume                          |
| Ana mkono mkono       | mwizi  |
| Jongoo hapandi mtungi | mwanaume aliyekosa nguvu za kiume                          |
| Mvua                  | damu ya mwezi  |
| Kupunguzia            | kupata damu ya mwezi ukiwa na mimba                        |
| Mjukuu                | kutu ya ntoto mdogo  |
| Mchezo                | tendo la ndoa  |
| Kupiga jicho          | kudhuru(husda)   |
| Ana ulimi             | mtu mwenye sifa ya kutukana au mgomvi                      |
| Hana maskio           | mtu asiyesikia la kuambiwa                                 |
| Pana mkono wa mtu     | pamerogwa  |
| Msalani               | chooni   |
| Kibogoyo              | mtu asiye meno   |
| Wamefungasha          | wamefuatana  |
| Ndwele                | ugojwa usiopona  |
| Zingizi               | ugonjwa wa tumbo baada ya kuzaa au kupata<br>damu ya mwezi |
| Uesa                  | umbea  |
| Uchoko                | uroho  |
| Ubuku                 | tabia ya udokozi   |
| Kuomoa                | kuzua/uzushi   |

|        |                          |
|--------|--------------------------|
| Midadi | nyege/hisia za kimapenzi |
| Ushi   | utupu                    |

#### **4.2.4 Tafsida Zinazozungumzwa Kazini**

Nikweli kwamba katika jamii inayotumia lahaja kama jamii ya wapemba, tafsida tofauti hutumika katika kazi, kupitia mchakato huo wapemba hutumia tafsida ili kuhifadhi nyuso za wafanyakazi wanapokuwa kazini. Tafsida 9 zilipatikana sawa na asilimia 23.52 ya tafsida zilizokusanywa. zifuatazo ni tafsida zinazotumika katika kazi.

| <b>TAFSIDA</b>  | <b>MAANA</b>                     |
|-----------------|----------------------------------|
| Anguka/Garagara | kuweka saini                     |
| Pumba           | kitu kisicho na hadhi/kisichofaa |
| Mkia wa mbuzi   | mshahara mdogo                   |
| Kizondo         | mtu mwenye uelewa mdogo          |
| Kilaza          | mtu asiye elewa                  |
| Chochote        | rushwa                           |
| Kutilia mguu    | kuchochea kitu kwa ubaya         |
| Mzito           | mtu asiye elewa                  |
| Mshiko          | pesa                             |

#### **4.3 Kupambanua Matumizi ya Tafsida Zinazotumika katika Lahaja ya Kipemba**

Lengo mahsusi la pililinasema, Kupambanua matumizi ya tafsida zinazotumika katika lahaja ya kipemba. Lengo hilililiongozwa na swali lisemalo. Ni yepi matumizi ya

tafsida hizo? Swali hili lilijibiwa na Watafitiwa thelathini (30) sawa na asilimia 85 na walieleza kuwa yapo matumizi ya tafsida, ambapo Wapemba wanayatumia katika mazungumzo yao kulingana na mazingira. Baada ya kuchunguza data, mtafiti aliweza kuzichambua data kwa kuongozwa na nadharia ya simiotiki inayojihusisha na ufumbaji na ufumbuaji wa mafumbo kwa kuelezea nini kimefumbwa au kiliashiriwa katika tafsida, kama zilivyojitokeza kwa watafiti wawalioteuliwa. Mtafiti alitaka kujua matumizi ya tafsida zinazotumika harusini, msibani, nyumbani na kazini, kwa kuanzia na matumizi ya tafsida zinazotumika katika mazingira ya harusini kama ifuatavyo:

#### **4.3.1 Matumizi ya Tafsida katika Mazingira ya Harusini**

Kwa kuanzia na matumizi ya tafsida za harusini ambapo Watafitiwa walieleza kuwa katika harusini tafsida hutumika kwa kuchangamsha hadhira iliyopo kama ifuatavyo:

“*Mtaimbo*” ni chuma kirefu chenye ncha kali, hutumika kufulia nazi pia kuchimbua sehemu zilizo ngumu. Matumizi yake hufananishwa na sehemu siri ya M’me (uume). Wapemba hutumia tafsida hii wawapo harusini kwa kuimba wimbo wa kuchangamsha harusini hapo.

“*Nimeshaupeleleza ntaimbo wateleza ntaimbo,*

*Uouo hauna malaika, uouo hauna malaika,*

*Nishaupeleleza ntaimbo wateleza ntaimbo.*”

Neno *mtaimbo* linapotajwa na wahuska (Wapemba) sauti “*m*” hubadilika na kuwa “*n*” kuonesha dhahiri matamshi ya lahaja ya Kipemba. Tafsida zenye maana sawa na hiyo ni: -*kijiti, Muwa.*

“*Kigozi manyoya*” Ni sehemu ya siri ya mwanamke iliyofanansihwa na ngozi yenye manyoya, tafsida hii hutumika kuonesha sehemu ya siri ambapo huambiwa harusini wa

kike kutokwenda kinyume na lengo la kuolewa kwake kwa kukataa kufanya tendo la ndoa na mumewe .Wanaharusi huimba wimbokwa kutaja tafsida hiyo kwa lengo la kumfunza harusiwao. Huu ni ushahidi wa mtafitiwa alipolezea tafsida hii.

*“Bei ya kanga waijuaaaa siijui,*

*Bei ya Mchele waijuaaaa siijui,*

*Bei ya Kabati waijua aaa sijuui,*

*Usijennyima dada wewe usijennyima **kigozi manyoya.***

Kutaja Kanga, Mchele, kabati ni moja kati ya vitu anavyovitafata m’me kumpa mkewe kwa gharama yoyote ile. Hivyo na yeye asijemnyima edapo atataka tendo la ndoa.

*“Kuchukaujiko”* Tafsidahiinatumiwa kwa m’me kuoa,Mfano wa mazungumzo ya tafsida hiyo ni Ali anachukau jiko leo. Ikimaanisha Ali ameo au anaoa na leo (anachukua mke) Neno jiko limefananishwana M’ke kwa ile sifa yake ya kupika akiwa nyumbani.Tafsida zenye maana sawa na hizo ni:- *kuasi ukapera, kujitwika mzigo.*

*Kungwi* “Ni mwalimu wa Maharusi hususan harusi wa kike ambapo hufuataniwa nae mtu huyo pale mmoja wapo anapoolewa na kuelekea kwake. Mafunzo anayoyatoani mambo ya siri yahasuyo maisha ya ndoa kwa bibi na bwana. Hivyo kwa Wapemba humwita *kungwi* kwa kuepuka kutamka maneno ya aibu kama kusema mwalimu wa maharusi wa mambo ya siri ya ndoa.

*“Somo”* Neno somo lina maana mbili, kwanza linatumika kama watu wawili waliofanana majina yao, Mfano Watu wawili wanaitwa jina *Maryam Juma* au kwa jina la mwanzo tu hawa watakuwa mtu na somo yake. Maana ya pili ni Mwalimu

wa mwanamke (Msichana) aliyepata ukubwa, aliyekuwa mwari, Mwalimu huyu humfunza Mwari(msichana) juu ya kuishi maisha ya ujari au utu uzima na athari zake na faida zake, pia humfunza juuya kukaa na watu hususan wanaume kwa sababu wakati umefika wakuwa na mahusiano baina ya mwanamke na mwanamme. Hivyo basi Wapemba humwita somo kuepusha maneno hayo, pia kuelewana baina ya wazungumzaji.

“*Jambo*” ni tafsida inayotumika kuonesha (kumanisha) tendo la ndoa Jambo ni neno tu kama maneno mingine ambalo limepewa uzito wa kitu kikubwa chenye umuhimu au kushitua. Mfano wa matumzi yake. *Ata ukimuona kamfurahi ujue atake jambo.*

*Nakwambia leo kampata jambole acheka tu.*

“*Mvua inanyesha*” “Hii ni tafsida ya mwanamke kutokwa na damu ya mwezi, imefananishwa na mvua kwa kilekinachoonekana kwa mwanamke ifikapo kipindi hicho anakuwa chabachaba(maji maji) katika uke wake. Mfano Alipofika kwake ilikuwa *mvua inanyesha.*

*Harusi wetu ananyeshewa na mvua. Mazungumzo haya huzungumzwa wakati shuhuli ya harusi inaendelea kama ni moja ya mazungumzo.*

“*Kachumbari*” Ni shanga za kiuno wanazovaa kina mama kwa ajili ya kupendezesha kwa waume zao. Zimeitwa kachumbari kwa sababu zinafanya kazi kama ya kachumbari ya kunogesha chakula ili kiweze kulika vizuri. Hivyo Wapemba hulitumia jina la kachumbari badala ya shanga za kuvaa kiunoni.

Tafsida nyingine na kama vile

“Mnyumba” – Mume au mke wa mtu. Mfano, *Yule ni mnyumba wake*.

“Wamelala” – kufanya tendo la ndoa, tafsida yenye maana sawa na hiyo ni :-

Mchezo

Wamepumzika

Kukutana

Tafsida za hapo juu zimepambanuliwa matumizi yake jinsi zinavyotumika katika jamii ya wapemba, pia imeonekana kutumika tafsida zaidi ya moja kuwa na maana moja .

#### **4.3.2 Matumizi ya aTuria katika Mazingira ya Nyumbani**

*Ana wageni:* Ni tafsida inayokusudia kuficha neno la karaha la mwanamke kupata damu yake ya kila mwezi. Tafsida nyigine zinakusudia kueleza muktadha huu ni kama vile:-

*Mchafu*

*Yuko kwenye siku*

*Mvu*

*Kutumia*

Mifano ya tafsida hizi ni:-

- Hawezi kufanya ibada kwa sababu ni *mchafu*.

- Alimkuta yuko *kwenye siku zake*

- Ananyeshewa na *mvua*

- Anaonenaka bado *anatumia*

- Yule ameshazeka *hatumii tena*

*“Mkono wa shati”*Tafsida inayokusudia kuonesha mwanamme ambae hawezi kufanya tendo landoa , umechukuliwa mkono wa shati pale ambapo ikiwa haijavaliwa unakuwa legevu. Hivyo umefananishwa uume na mkono wa shati.

Tafsida nyingine inayokusudia kutaja hali hii ni kama vile:-

*Jongoo hapandi mtungi.*

Mfano Yule nimkono wa shati.

Alikuwa *jongoo hapandi mtungikwa* muda mrefu sasa.

*“ Mja mzito ”* Ni tuaria inayotumika kuonesha mtu mwenye mimba. Mja mzito ni neno lenye kuonesha mtu mzito yaani “mja” ni kiumbe au mtu na “mzito” ni kuongezeka uzito kuliko ule wa kawaida. Hivyo imechukuliwa mimba kuwa ndio uzito na kusema mja mzito.

*“Ukama”* Ni tafsida inayotumika kuonesha uzi wa kiuno anaovalishwa mtoto au hata mtu mzima, utanzi auushanga unavaliwa kiunoni.

*“Kujifungua”* Ni tafsida inayotumika kuonesha kuzaa: imetumika kujifungua kuficha neno kuzaa kwa sababhu kujifungua imeonekana inaficha hisia zamtu kuelekeza akili yake moja kwa moja na tendo lenyewe, badala yake imetumika kujifungua ili kupunguza aibu hiyo

*“Kufunduwa”*Tafsida hii hutumika kwa kuonyesha kuota maziwa au machuchu, (matiti) kwa m’ke ambae anaingia umri wa kuwa mkubwa (Mwari), linatumika neno kufundua badalaya kuota machuchu (maziwa).

*“Ujusi”* Ni tafsida inayotumikakuonyesha M’ke anaetokwa na damu baada ya kujifungua.

“*Barua*” Talaka, neno talaka hufichwa kuficha aibu ya m’ke kuachwa na kutumika neno la barua ambalo linaonekana ni neno la kawaida ambapo barua ni karatasi iliyobeba maadishi yenye ujumbe mzito ndani yake.

“*Mwega*” Ni tafsida inayotumika kuonesha vazi la sidiria. Neno mwega limechukuliwani kitu ambacho hutumika kuegemeza kitu ili kisianguke. Hivyo basi imechukuliwa sidiria kuwa ni mwega wa maziwa (Machuchu) yaliyolala kuegemezwa kwa kurudishwa katika hali yake ya mwanzo.

“*Kufuli*” Ni tafsida inayotumika kuonesha vazi la chupi, imeonekana kuwa kusema chupi nineno linaloleta aibu pale ambapo mtu ataielekeza akili yakena pale inapovaliwa. Hivyo hutumikaneno kufuli likimanisha kukomea sehemu muhimu.

“*Kujisaidia*” ni tuaria inayotumika kuonesha kunya au kukojoa. Kutokana na maneno haya huleta fikra nyinge wakati wa kulitamka, fikra hiyo huonekana ni uchafu au karaha. Hivyo kuepusha hilo, neno kujisaidia huchukua nafasi badala ya kunya au kukojoa.

“*Kutabaali au kubaua*” ni tafsida zinazotumika kuonyesha kitendo cha kukojoa.

“*Ana mkonomkono*” Tafsida inayotumika kuonyesha tabia yamtu kuwa mwizi. Hivyo hutumika neno mkonomkono kuepusha migongano badala ya kusema ni mwizi.

“*Kupunguzia*” ni tuaria ambayo hutumika kuonyesha M’ke mwenywe mimba ambae anapata damu yake ya kila mwezi. Hivyo hutumikaneno kupunguzia kuonesha hiyo hali na kupunguza ule ukali wa maana ya nen hilo.

“*Kupiga jicho*” Ni tafsida inayotumika kuonyesha kuhusudi (husda), ni Kule kukiangalia kitu kwa lengo la kudhuru.

“*Ana ulimi*” Ni tafsida inayoonyesha tabia ya mtu anaependa kusema maneno ya ukali, ujeuri, matusi, pia mtu huyu huitwa “Fidhuli”. Hivyo limechukuliwa neno ulimi



kuonesha ndio kiungo kikuu cha utamkaji wa maneno vikisaidiana na vyingine kama vile meno, midomo, mafizi n.k.

*“Pana mkono wa mtu”*Tafsida hii huonyesha hali ya kuroga. Hutumikaneno mkono wa mtu kuonyesha watu ndio wenye tabiaya kuroga, kuepusha hisia kali pale utakaposema kuroga na badala yake kupuguza hisia hizo kwa kusema pana mkono wa mtu.

*“Wamefungasha”* Ni tafsida inayoonyesha kitendo cha kufuatana mtu na mke au mume wake, huambiwa wanafungasha kwa lengo la kuafuatana.

*“Ndwele “* ni tafsida inayoonyesha maradhi yasiyopona ambayo huchukua muda mrefu hadi kupona maradhi hayo.

*Zingizi*, ni maumivu ya tumbo anayoyapata mke mara tu baada ya kujifungua au anapopata damu ya mwezi.

*“Usesa”*ni tabia ya kuchunguza mambo ya watu yasiyokuhusu.

*“Uchoko”*tafsida hii hutumika kuonyesha tabia ya uroho.

*“Ubukwa”* ni tafsida inayoonyesha tabia ya mtu kudokoa chakula jikoni na kula kwa kujificha kabla hakijapakuliwa,hutumika neno mbukwa badala ya mdokozi.

*“Kuchopa/kutomasa”*ni tafsida inayoonyesha kubonyezwa kwa vidole sehemu zinazoleta hisia.

*“Nchopi”*ni tafsida inayoonyesha mtu mgomvi/mchokozi.

Matumizi ya tafsida za hapo juu zinaonekana kwa kiwango kikubwa kuwa ni tafsida zinazozungumzwa katika mazingira ya nyumbani ingawa zipo baadhi ya tafsida zinazungumzwa katika mazingira ya harusini,pia imeonekana kuwa maana moja ya tafsida imewakilishwa na tafsida zaidi ya moja.

### 4.3.3 Matumizi ya Tafsida katika Mazingira ya Msibani

Tafsida za msibani ni tafsida zinazotumika kwa lengo la kupunguza majonzi, simanzi au kutoa ushirikiano wa kimsiba kwa kuwafariji wote waliopata msiba. Miongoni mwa mifano ya tafsida hizo ni hizi zifuatazo ambapo Mtafiti alizipata baada ya kuwahoji Watafiwa wake.

*Faradhi* ni tafsida inayotumika kuonyesha kifo,limetumika neno faradhi kuonyesha ni kitendo cha lazima ambapo kila mmoja kitendo hicho cha kufa kitamfika,Wapemba hilitumia neno hili kupunguza majonzi kwa wafiwa ili wajione na wao ipo siku litawakuta.

Mfano, Mwambie baba yako tumepata *faradhi*.

Tafsida nyingine zenye maana kama hiyo ni:-

- *Ametanguli mbele ya haki*
- *Tumepata msiba*
- *Mgonjwa amemaliza*
- *Amehitajika*
- *Amefika hatma*
- *Amekwenda kuzimu*

“*Malaloni*”ni tafsida inayoonyesha kitendo cha mtu kuzikwa kaburini,hii imefananishwa na kitendo cha kulalakwa kule kutokwa na akili na ufahamu kupotea(amelala).

“*Mavani*”nitafsida inayoonyesha sehemu ya watu wanapozikwa.

“*Tusi*”nitafsida inayoonyesha kifaa cha kuchukulia maiti anapokwenda kuzikwa(mavani),kifaa hicho kinajulikana kwa jina la *jeneza*,hivyo imeonekana neno jeneza ni neno linaloleta mshitukoutakapolitamka na badala yake hutumika neno tusi kuepusha hali hiyo.

#### 4.3.4 Matumizi ya Tafsida katika Mazingira ya Kazi

“*Anguka*” ni tafsida inyoonyesha kuweka saini.

“*Pumba*” nitafsida inayotumika kuonyesha kitu kisichoeleweka, imchukuliwa neno pumba kwa maana ya kumvi ambazo hazifai tena.

Mfano, Alichokizungumza *nipumba* tupu.

“*Mkia wa mbuzi*” ni tafsida iyoomaanisha mshahara mdogo.

“*Mshiko*” ni tafsida inayotumika kuonyesha mshahara.

“*Kizondo*” ni tafsida inayotumika kuonyesha mtu asiyelewa mara moja.

Hivyo hali hii inaonesha kuwa tafsida zinazotumika katika mazingira ya kazi hazitumiki kwa kiwango kikubwa hali ambayo imedhoofisha tafsida kwa kile kinachoonekana kuwa katika kazi watu wanaonekana kuwa na hadhi zawa lakini pia rika sawa.

#### 4.4 Kuelezea Faida na Hasara ya Matumizi ya Tafsida katika Jamii Hususani Jamii ya Wapemba

Lengo hili liliongozwa na swali linalosema; Jee tafsida zina faida na hasara katika jamii? Miongoni mwa Watafitiwa 35 walioulizwa swali hili, watafitiwa 28 tu ndio waliojibu swali hili sawa na asilimia themanini 80%, wakiwemo wanawake 18 na wanaume 10 vijana na wazee wenye hadhi tofauti ya Kielimu, majibu ya swali hili yalikuwa kama ifuatavyo:-

Kwa kuanzia na faida

#### **4.4.1 Faida ya Matumizi ya Tafsida katika Jamii**

Baada ya mchakato wa kuuliza maswali juu ya faida na hasara ya kutumia tafsida katika lahaja ya kipemba. Matafiti aligundua kuwa matumizi ya tafsida yanaweza kuwa na faida zifuatazo:

Kwanza, kuondosha migongano ya kiutamaduni. Tuki (2004) inasema “Utamaduni ni mila, jadi na desturi za kundi Fulani. Utamaduni wa Wapemba ni pamoja na kuheshimiana baina yao. Hivyo kutumia tafsida katika jamii kutaepusha migongano kwa kutunza heshima hiyo na isipotumiwa vyema itapelekea jamii kuzozana. Mfano wa tafsida hizo ni pamoja na usesa, sheria, ana wageni nk.

Aidha, hupelekea kuepuka kutaja na kutumia maneno yenye aibu na yenye miiko katika jamii. Katika kufanikisa mawasiliano kilamtumizi wa lugha hutumia tafsida ilikuonyesha kuwajali kuwaheshimu na kuwatambua wengine kwa kutaja tafsida zinazofanya mazungumzo yaendeleo kuzungumzwa. Mfano, Hawajakutana. Mkono wa shati, Kachumbari, kufuli. Yuko kwenye siku.

Pia, tafsida zinatoa miongozo ya kiutamaduni. Hii ni kwamba wakati mwingine matumizi ya tafsida hutoa miongozo kwa kuwafunza na kuwaelekeza baadhi yao juu ya kile wasichokijua. Mfano tafsida ya “Ana macho ya nje” inaonesha dhahirikwa wale ambao hawaridhiki na wake zao mpaka wapate na Wanawake wasiohalali kwao. Hivyo tafsida hii inatoa mwongozo wa kuishi na wake zao na sio kutafuta w’ke wasiohalali kwao, tafsida nyingine ni kama vile ubuku. Usesa Uchoko, ana ulimi n.k. Vilevile, watafitiwa walisema kuwa tafsida huweza kukuza lugha, Kwa kutumia tafsida wanajamii wataikuza na kuiendeleza kwa kuingiza maneno yasiyozoeleka ili

kuzoeleka katika lugha. Hivyo lugha itakuwana tajiri kwakupata maneno mapya na kupelekea kukua siku hadi siku. Mfano wa Tafsida hizo ni kizondo, Uchoko, Kibogoyo, Ubuku, Pumba, Ukama nk.

Mwisho, tafsida zinajenga umoja na mshikamano. Kupitia matumizi ya tafsida jamii inajenga umoja na mshikamano kwa kuonesha kujaliana, kupendana na hata kushirikiana pale wanapokuwa katika jamii kwa kutumia tafsida zinazofaa kulingana na mazingira waliyo na pia kujuana kwamba wao ni kitu kimoja. Hivyo mara tu wanapotumia huelewana nini kimekusudiwa kuonesha wote ni kitu kimoja/wamoja.

#### **4.4.2 Hasara ya Matumzi ya Tafsida katika Jamii**

Mtafiti pia alipata kuhoji kuhusu hasara zinazoweza kusababishwana tafsida na kupata majibu yafuatayo:

Kwanza, tafsida zinawatenga miongoni mwa wanalugha. Hii ina maana kwamba wapo baadhi ya wanajamii ambao hawajui tafsida, hivyo wanapokutana nazo katika mazungumzo wanashindwa kuelewa ni kitu gani kimekusudiwa na hupelekea kuachwa nyuma kimawasiliano ama kutofahamu nini kimekusudiwa au kwa kutoelewa kama na wao wamejumuisha kimazungumzo. Mfano wa wanalugha hao ni kizazi kipya ambao hawaelewi tafsida za zamani kutokana na kutotumia tafsida hizo.

Pia, ilielezwa kuwa tafsida zinaweza kusababisha migogoro kwa jamii. Kama ilivyokishaelezwa kwamba kila jamii ina mila na desturi zake inazotumia, endapo jamii haikutunza mila na desturi migogoro na migongano itatokea. Kwasababu itaondoa pia ule ustaarabu wa mazungumzo kwa kutumia lugha nzuri ya heshima ili kusitiri nyuso za wanajamii, ili kufanikisha hilo lazima tafsida zitumike katika jamii hususan jamii ya wapemba.

#### **4.5 Hitimisho**

Katika sura hii mtafiti amechambua malengo ya utafiti kama yalivyoonekana katika utafiti huu na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Malengo hayo ni pamoja na Kubaini tafsida zinazotumika katika lahaja ya Kipemba, Kupambanua matumizi ya tafsida zinazotumika katika lahaja ya Kipemba, mwisho Kuelezea faida na hasara za matumizi ya tafsida hizo katika jamii ya Wapemba. Utafiti unaonesha kwamba malengo yote hayo yamefikia matarajio yake ya kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba na kutoa matokeo yake katika sura ya tano.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI WA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii inahusiana na hitimisho la utafiti huu kwa ujumla kwa kuelezwa Muhtasari wa kazi hii ambao umechukua baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika kila sehemu, utumiaji wa nadharia zilizotumika katika utafiti huu na jinsi ulivyosaidia katika uchambuzi wa data zilizopatikana na mwisho sehemu hii imebanisha maoni na mapendekezo yaliyotolewa na mtafiti wa utafiti huu.

#### **5.2 Muhtasari wa Utafiti**

Utafiti huu umegawika katika sura tano, kila sura imejitosheleza kwa kueleza vipengele muhimu vinavyojitegemea. Sura ya kwanza imeelezea usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti huu, malengo na maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na hitimisho la sura hiyo.

Sura ya pili ilikuwa inahusiana na mapitio ya kazi tangulizi na imefafanua dhana ya Semi katika kipengele cha tamathali za semi (tafsida) kwa ujumla na mapitio ya kazi zilizowahi kufanywa kuhusiana na mada hii kutoka kwenye tafiti na vitabu mbali mbali. Kazi zilizopitiwa ni pamoja navitabu, makamusi na tasnifu ambazo zimemsaidia mtafiti kuweza kupata mada hii ya utafiti, baada ya kugundua kuwa hakuna Waandishi waliowahi kujitokeza kuandika kwa kina kuhusu mada hii yakuchunguza matumizi ya mafsida katika lahaja ya Kipemba. Pengo la utafiti na mkabala wa nadharia iliyotumika katika utafiti huu zilibainishwa katika sura hii. Sura ya tatu imejadili mbinu ya utafiti huu. Pia sura hii imeelezea eneo lililotumika katika

utafiti huu. Sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data pamoja na kuchambua data na vifaa vya utafiti. Sura ya nne imeelezea mchakato mzima wa ubainishaji wa tafsida zinazotumika katika lahaja ya kipemba, matumizi ya tafsida za lahaja ya kipemba pamoja na faida na hasara za matumizi katika jamii ya Wapemba. Sura ya tano ambayo ya mwisho, imeeleza kwa ufupi mchakato mzima wa utafiti mpaka kufikia ugunduzi wa yale yaliyojitokeza juu ya utafiti. Vile vile sura hii imebainisha mapendekezo na maoni ya mtafiti baada ya utafiti kukamilika.

## **5.2.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti**

### **5.2.1.1 Lengo la Kwanza**

Lengo hili liliongozwa na swali lisemalo ,Ni tafsida zipi zinazotumika katika lahaja ya Kipemba? Swali hili lilijibiwa kwa kuorodhesha tafsida hizo zinazotumika katika lahaja ya Kipemba kama zilivyoonekana katika kifungu 4.2.Mtafiti amegundua kuwa Wapembakupitia lahaja yao ya kipemba wanazo tafsida zinazotumika katika lahaja hiyo.Pia tafsida hizo zimegawika katika makundi manne nayo ni:-

Tafsida zinazotumika msibani

Tafsida zinazotumika harusini

Tafsida zinazotumika nyumbani

Tafsida zinazotumika kazini.

### **5.2.1.2 Lengo la Pili**

Lengo hili liliongozwa na swali lisemalo,Ni yepi matumizi ya tauria hizo? Katika kujibu swali hili mtafiti aligundua kuwa katika matumizi ya tafsida zinazotumika katika lahaja ya Kipemba yazimekusanya mafunzo maelekezona hata busara ya



kutumia maneno hayo ili kuleta heshima ya mazungumzoni kuficha aibu kwa msilizaji.

### **5.2.1.3 Lengo la Tatu**

Liliongozwa na swali lisemalo,Je, tafsida zina faida na hasara gani katika jamii? Kupitia jawabu ya swali hili mtafiti alibaini kuwa ni kweli tafsida zina faida na hasara katika matumizi yake. Kwa upande wa faida ni pamoja na kuondoa migongano ya kiutamaduni, kuepuka kutaja maneno yenye aibu na miiko katika jamii,zinatoa miongozo ya kiutamaduni lakini pia inakuza lugha..pia mtafiti aligundua hasara ya matumizi ya tafsida hizo ni pamoja na kuwatenga miogoni mwa wanalugha, kusababisha migogoro katika jamii.

Kwa ujumla mtafiti amegundua kuwa, kataika utafiti huu Wapemba wanazo tafsida zao wanazozitumia kupitia lahaja yao ,pia amegundua matumizi hayo yanaleta heshima na upole wakati wa mazungumzo,lakini pia kuficha aibu na kulinda uso wa msikilizaji .Vilevile matumizi ya tafsidahizo yanashawishi umoja na mshikamano katika jamii ya wapemba,lakini huchochea mizozo na migongano ambapo hii ni hasara katika jamii.

## **5.3 Mapendekezo**

### **5.3.1 Mapendekezo ya Jumla**

Kutokana na matokeo ya data tulizokusanya tumeona kwamba matumizi ya tafsida ni muhimu sana katika kila jamii kwani kila jamii inafanya juhudi za kuimarisha na kuendeleza maadili. Hivyo basi tunapendekeza tafsida za lahaja ya kipemba ziendele kutumika.

Pia ziandikiwe kamusi kwani maneno mengi yanaendelea kufa na kuathiriwa na lugha za kigeni. Tunapendekeza pia waandishi wa vitabu vya shule za msingi na sekondari waongeze mada za tafsida katika vitabu vinavyotumiwa mashuleni na katika vyuo, kuongeza mada kutawapa wanafunzi wengi matumizi bora ya tafsida.

Matumizi ya tafsida hulenga kurahisisha mawasiliano, kuwasiliana kwa njia muafaka kuhifadhi aibu ya msikilizaji ili kuweza na kuwasiliana kwa upole. Hii tumependekeza kwa sababu ya kuwepo na sera inayomgusa mwanadamu kutilia mkazo mafunzo ya tafsida. Sera kama za elimu za matibabu, biashara na mashirika binafsi kuzingatia mafunzo ya tafsida kwani kutapunguza chuki, migongano na mifarakano zinazoletwa na kutofautiana kwa mazungumzo na lugha isiyo ya kificho.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza matumzi ya tafsida katika lahaja ya Kipemba, ambao ulifanywa kwa kuzingatia mazingira ya nyumbani zaidi. Utafiti mwingine unaweza kufanywa katika muktadha mbali mbali inayohusu shughuli mbali mbali za binadamu kama vile matibabu, shuleni, vituo vya magari, sokoni michezoni nk. Lakini pia kupitia lahaja nyingine kama vile Kitumbatu, Kimakunduchi au hata lugha za kimakabila kama vile Kichaga, Kimakonde Kisukuma n.k.

### **5.3.2 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo**

Kama ulivyoonekana kuwa utafiti huu umefanyika katika kisiwa cha Pemba tu, na Zanzibar ni muunganiko wa visiwa viwili yaani Unguja na Pemba. Hivyo ni vyema kabisa tafiti zijazo katika kisiwa cha pili cha Unguja ili kuweza kupata idadi kubwa zaidi ya tafsida kwa upande wa lahaja, ili zihifadhiwe kwa ajili ya kizazi (wasomi)wajao.

Vilevile katika utafiti huu imebainika kuwa tafsida zina faida mbalimbali katika jamii ya Wapemba, ambapo faida hizo zinafanikisha mustawa mzima wa maisha ya Wapemba. Hivyo tafiti nyingine zifanyike kupitia lahaja nyingine ili kuleta urahisi wa mawasiliano na pia kuleta utajiri wa maneno kwa wasiojua lahaja nyingine

#### **5.4 Hitimisho**

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya tafsida/tafsida katika lahaja ya Kipemba. Utafitia huu ulikuwa na lengo la kuchunguza jinsi matumizi ya tafsida ya lahaja ya kipemba hufanikisha mawasiliano na iwapo hali za kijamiikama umri, jinsia, kazi na hadhi huathiri matumizi ya tafsida hizo. Utafiti ulikuwa na lengo la kujibu maswali makuu matatu:

- (i) Ni tafsida zipi zinazotumika katika lahaja ya Kipemba?
- (ii) Ni yepi matumizi ya tafsida hizo katika lahaja ya Kipemba?
- (iii) Je, tafsida zina faida na hasara gani katika jamii?

Kutokana na matokeo ya data imedhihirika kwamba matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba hutumika kwa sababu ya kuleta heshima katika jamii, yaani jamii kupata fursa ya kuheshimiana wenyewe kwa wenyewe. Pia ibainike kuwa tafsida nyingi zimeundwa kutokana na vitu, vifaa na hata hali zilizomo katika jamii dhidi ya mazingira yaliyowazunguka. Matumizi ya tafsida za aina tofauti kama vile sehemu za siri za mwili wa binaadamu, hedhi, kifo yalikuwa na uhusiano mkubwa. Hii ni kwa sababu watumiaji wa tafsida hizi walidhihirisha kwa asilimia kubwa kutumia tafsida kwa kuashiria vitu hivyo kwa kiwango kikubwa.

Jamii ya Wapemba pia ilidhihirisha kutumia tafsida zilizofanana kwa kuashiria kitu kimoja, Mfano *damu ya mwezi kwa m'ke(hedhi)*, ilitumika kwa kupata siku, kutumia,

Mvua ana wageni n.k. katika *kifo* hutumika pia tafsida kama ametangulia mbele ya haki, ametutoka, faradhi n.k. *Kujifungua* hutumika pia tafsida ya kufika pwani, kupongoa n.k.

Uchunguzi umeona kwamba tafsida nyingi huzungumzwa katika mazingira ya nyumbani ambapo tafsida zinazohusu tendo la ndoa/ kujamiiana huzungumzwa kwa wingi pamoja na zile zinazohusu maswala ya wanawake, hii kwa sababu tafsida hizi huonekana za aibu sana kuliko tafsida nyingine katika jamii.

Kwa ujumla tafsida zilitumika ili kuhifadhi uso kwa msikilizaji na kufanikisha mawasiliano pasipo kuoneana aibu kwa wasikilizaji kwanjia yakuashiria kitu. Uchunguzi huu umeonyesha shughuli za kijamii kama vile harusi, msiba, kazi na hata mazingira ya nyumbani ambapo tafsida hutumika, ingawa shughuli za kikazi na harusi huathiri sana matumizi ya tafsida kwani shughuli hizo mara nyingi hukusanya watu wenye umri sawa, cheo kimoja na watani na kupuuza matumizi ya tafsida ambayo imeonekana heshima katika shughuli hizo ni ya kiwango cha chini sana.

Vile vile uchunguzi huu uligundua kwamba matumizi ya tafsida za nyumbani ni kwa ajili ya kupunguza makali na kuhifadhi uso wa wazungumzaji kwa kuficha kile kitu halisi kilichokusudiwa kwa kufumba fumbo. Haya yanadhihirika kupitia nadharia ya simiotiki ya Fredinand Dessausare (1970) inayoshughulika na ufumbaji na ufumbuzi wa mafumbo katika kazi ya fasihi. Hii ina maana kwamba watu wakizungumza katika jamii hufuata sheria za mahali wanapozungumza ili kuepusha migongano, kama vile Wapemba wanapotumia tafsida katika kuwasiliana wakizingatia mazingira walipo kwa kuzingatia ubunifu wa mazungumzo hayo.

## MAREJELEO

- Allan, K., and Burrige, K. (1991). *Euphemism and Dysphemism*. New York:Oxford University Press.
- Babbie, E. (1999). *The basic of research*.Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- BAKIZA, (2008). *Utamaduni wa Mzanzibari*. Zanzibar: QuarkXpress, Printing Services.
- BAKIZA, (2012). *Kamusi ya Lahaja ya Kimakunduchi*. Dar es Salaam: Jamaa Printers Ltd.
- BAKIZA, (2012). *Kamusi ya Lahaja ya Kipemba*.Nairobi: Exford University Press.
- Best, W. R. (1996). *Educational Research an Introduction*: New York. Longman.
- Bukagile, G., and Yogo, M. (2010). *Theory of literature*. Dar es Salaam.
- Chacha, L. M., and Ngugi, P. (2004). *AKS 400: Sociolinguistics*. Nairobi: Institute of Open Learning Kenyatta University.
- Enon**, J. C. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurement*, Kampala: Makerere University.
- Gatambuki, M. G. (2010). *A cognitive Linguistic Analysis of Gikuyu Euphemisms*. M.A Kenyatta University. Unpublished thesis, Nairobi, Kenya.
- Gibbe, A. G. (1980). *Mitaala ya Lugha na Fasihi*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Hrry,H.(1954).*Language in Clture*.Chicago:The University of Chicago Press.
- Hymes, D. (1964). *A Language, Culture and Society*. New York: Harper and Row Publishers.
- Ingram,W.H.(1931). *Zanzibar Noteson the Dialects*.London, Longman.

- Ingram, W. H. (1924). The Dialects of Zanzibar Sultanet in Bulletin of School of Oriental and African Studies. *London Journal African Studies*, 3(3), 533-550.
- John, J., na Mduda, F. (2012). *Kiswahili kidato cha 5 - 6*: Dar es Salaam: Oxford University Press (T) Ltd.
- Kombo, D. K., and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and thesis writing, Introduction*. Nairobi. Paulines Publication Africa.
- Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern.
- Kothari, R. C. (2004). *Rsearch Methodology, Methods and Technique (2<sup>nd</sup> ed.)*. New Delhi: New Age International (P) Limited Publishes
- Masebo, J. A., na Nyangwine, N. (2004). *Nadharia ya fasihi Kiswahili 2 kidato cha 5,6*. Dar es Salaam: General Supplies Ltd.
- Mde, S. J. (2014). *OSW 613: Isimu Jamii*. Dar es Salaam: Dar es University Press.
- Mukaria, J. M. (2011). Misamiati ya Miiko na Tafsida katika Kiigembe. Tasnifu ya uzamili katika Chuo Kikuu Cha Nairobi, Haijachapishwa. Dar es Salaam, Tanzania.
- Mulokozi, M. M., na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Pubishing House.
- Nguti, M. (2013). Tasnifu ya Ulinganishi wa Matumizi ya Tafsida za Mukstadha wa Nyumbani Katika lugha ya Kikamba na Kiswahili: Chuo Kikuu Nairobi, Kenya.
- Njeri, S. (2007). A Pragmatic Analysis of Gikuyu Lexical Euphemism HIV/AIDS Discourse Unpublished M.A Thesis, University of Nairobi, Kenya.
- Saidi, M. (1976). *Fani mbalimbali za Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Kenya ltd.

- Senkoro, E. (1980). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Wambua, R. S. (2009). Variation of Dialectical use of and Attitudes toward Taboo Ward and Euphemism in Kikamba. Un Published M.A Project O.U.N. Nairobi, Kenya.
- Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi-Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd- Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi Litho Limited.

## VIAMBATANISHI

### **Kiambatanishi Na. I: Mwongozo wa Maswali ya Hojaji**

#### CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

Maswali ya hojaji ya kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba. Hojaji hii inalenga kukusanyataarifa za kuchunguza matumizi ya tafsida katika lahaja ya kipemba, kama unavyoelewa na kutumia lugha inayohusika. Majibu yatakuwa siri kati ya mtafiti na mtafitiwa, sio lazima kuandika jina lako katika hojaji hii.

#### **SEHEMU A:** Maelezo bafsi kuhusu Mtafitiwa.

1. JINSI M'K E ( ) MUME ( )
2. UMRI i) 60-80 ( ) (ii) 20-50 ( )
3. KIWANGO CHA ELIMU (i) msingi ( )
  - (ii) sekondari ( )
  - (iii) diploma ( )
  - (iv) shahada ( )
  - (v) sikusoma ( )
4. KAZI YAKO -----
5. CHEO CHAKO -----.



**SEHEMU B:** Hojaji kuhusu mada.

Tafadhali jibu maswali yafuatayo kwa kufuata maelezo uliyopewa.

6. Je, unazifahamutafsida? Ndio ( ) Hapana ( ).

7. Kama ndio, taja tafsida zinazotumika katika lahaja ya kipemba.

i) -----

ii) -----

iii) -----

iv) -----

v) -----.

8 a.) Katika mazingira gani wapemba hutumia tafsida ? Yataje.

i) -----

ii) -----

iii) -----

iv) -----

v) -----.

b) Taja tafsida zinazotumika katika mazingira uliyotaja.

i) -----: -----,-----.

ii) -----: -----,-----.

iii)-----: -----,-----.

i) -----: -----,-----.

ii) -----: -----,-----.

9. Ni yepi matumizi ya tafsida ulizozitaja?

Tafsida

Matumizi(maana)

|       |       |
|-------|-------|
| ----- | ----- |
| ----- | ----- |
| ----- | ----- |
| ----- | ----- |
| ----- | ----- |

10. Taja faida na hasara ya matumizi ya tafsida katika jamii.

Faida -----

-----

-----

-----

Hasara -----

-----

-----

-----

-----.

AHSANTE SANA

**Kiambatanishi Na. II:Usaili Kwa Watafitiwa Ambao Hawajui Kusoma na Kuandika**

**SEHEMU A.**Maelezo binafsi ya msailiwa.

1. Una umri/miaka mingapi?-----

Unaishi wapi?-----

Unafanya kazi gani?-----

**SEHEMU B.**Usaili kuhusu mada.

2. - Je, wewe ni Mpemba?

- Unafahamu nini unaposikia neno tafsida? Je, unazifahamu tafsida za kipemba zinazozungumzwa na wapemba?

- Nitajie tafsida unazozifahamu zinazotumika katika lahaja ya kipemba.

- Ni yepi matumizi ya tafsida hizo.

- Katika mazingira gani tafsida hutumika sana?

- Nitajie tafsida zinazotumika katika mazingira ya Harusini,Msibani,Kazini na Nyumbani.

- Je, kuna faida na hasara ya matumizi ya tafsida katika jamii ya wapemba?

- Nitajie hasara na faida ya matumizi ya tafsida katika jamii ya wapemba.

**AHSANTE SANA**

**Kiambatanishi Na. III:Kinaonyesha Orodha ya Tafsida na Maana Zake**

| <b>TAFSIDA</b>                               | <b>MAANA</b>                              |
|--|---|
| <i>Kuchukua jiko/kuasi ukapera/kujitwika</i> | <i>kuoa</i>                               |
| <i>mzigo</i>                                 | <i>kuwa mwari(msichana)</i>               |
| <i>Kuvunja ungo</i>                          | <i>kukojoa</i>                            |
| <i>Kutabaali/kubaua</i>                      | <i>kunya au kukojoa</i>                   |
| <i>Kujisaidia /kwenda haja</i>               | <i>chooni</i>                             |
| <i>Msalani</i>                               | <i>kuota maziwa</i>                       |
| <i>Kufundua</i>                              | <i>vazi la chupi</i>                      |
| <i>Kufuli</i>                                | <i>kuzaa</i>                              |
| <i>Kujifungua</i>                            | <i>vazi la sidiria</i>                    |
| <i>Mwega</i>                                 | <i>shanga za kuvaa kiunoni</i>            |
| <i>Kachumbari</i>                            | <i>mtu mwenye mimba</i>                   |
| <i>Mja mzito</i>                             | <i>mtu mvivu</i>                          |
| <i>Mzigo</i>                                 | <i>mtu mwenye ufahamu mdogo katika</i>    |
| <i>Kizondo</i>                               | <i>kusoma</i>                             |
| <i>Ukama</i>                                 | <i>uzi anaovalishwa mtoto kiunoni</i>     |
| <i>Pumba</i>                                 | <i>kitu kisicho na hadhi</i>              |
| <i>Kigozi manyoya</i>                        | <i>sehemu ya siri ya mwanamke(uke)</i>    |
| <i>Mtaimbo/muwa/kijiti</i>                   | <i>sehemu ya siri yamwanamme(uume)</i>    |
| <i>Mkono wa shati/jongoo hapandi mtugi</i>   | <i>ni mwanaume alikosa nguvu za kiume</i> |
| <i>/jogoo hawiki</i>                         |   |
| <i>Ana mkonomkono</i>                        | <i>mtu mwenye tabia ya wizi</i>           |
| <i>Yuko kwenye siku/mchafu/ana</i>           | <i>ni hali ya mwanamke anaepata damu</i>  |
| <i>wageni/mvuahedhi</i>                      | <i>ya kila mwezi</i>                      |
| <i>Ametanlia mbele ya</i>                    | <i>kitendo cha mtu kufa</i>               |
| <i>haki/faradhi/mgonjwa ametutoka</i>        | <i>makaburini</i>                         |
| <i>Mavani/malaloni</i>                       |   |
| <i>Tusi</i>                                  | <i>jeneza</i>                             |

|                              |   |
|------------------------------|---|
| <i>Barua</i>                 | <i>talaka</i>                               |
| <i>Kukutana/sharia</i>       | <i>kufanya tendo la ndoa</i>                |
| <i>Kiwembe/ macho ya nje</i> | <i>mtu anaependa kufanya ngono zembe</i>    |
| <i>Mnyumba</i>               | <i>mke au mume wa mtu</i>                   |
| <i>Kungwi/ somo</i>          | <i>mwalimu wa harusi wa kike</i>            |
| <i>Kupunguzia</i>            | <i>kupata damu ya mwezi ukiwa mja mzito</i> |
| <i>Kupiga domo</i>           | <i>kusema umbea</i>                         |
| <i>Kutilia mguu</i>          | <i>kuchochea kitu kwa ubaya</i>             |
| <i>Ulimi/fidhuli</i>         | <i>mtu mwenye kuzungumza kauli</i>          |
|                              | <i>mbaya/chafu za kukera</i>                |
| <i>Hana masikio</i>          | <i>mtu mkaidi</i>                           |
| <i>Pana kono wa mtu</i>      | <i>kuroga</i>                               |
| <i>Kibogoyo</i>              | <i>mtu asiye na meno</i>                    |
| <i>Wamefungasha</i>          | <i>kitendo cha mtu na mkewe kufuatana</i>   |
| <i>Ndwele</i>                | <i>maradhi yasiyopona(ugonjwa)</i>          |
| <i>Zingizi</i>               | <i>maumivu ya tumbo baada ya</i>            |
|                              | <i>kujifunguaau unapopata damu ya</i>       |
| <i>Chochote</i>              | <i>mwezi</i>                                |
| <i>Usesa</i>                 | <i>rushwa</i>                               |
| <i>Uchoko</i>                | <i>tabia ya umbea</i>                       |
| <i>ubuku</i>                 | <i>tabia ya uroho</i>                       |
|                              | <i>tabia ya udokozi</i>                     |

**Kiambatanishi Na. IV:Kinaonyesha Kisiwa cha Pemba Katika Eneo la Mkoa wa  
Kusini Pemba**



**Kiambatanishi Na. V:Kinaonyesha Eneo la Chake Chake Mjini Kisiwani Pemba**



**Kiambatanishi Na. VI:Kinaonyesha Kisiwa cha Pemba Ambapo Lahaja ya  
Kipemba Inazungumzwa**





**Kiambatanishi Na. VII:Kinaonyesha Shughuli Mbalimbali za Wananchi katika Eneo la Mjini Chakechake Pemba Ambapo Eneo Hili Ndilo Mtafiti alifanya Utafiti wake Kuwakilisha Pemba Nzima**

